

KUDHANIA



. . . amini tu.

² Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Kuna haja zozote, inua mkono wako na moyoni mwako useme, “Mungu, Wewe unajua yaliyo moyoni mwangu.” Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

³ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe, asubuhi ya leo, kwa ajili ya upendo wa kweli wa Mungu uliomiminwa ndani ya mioyo yetu na Roho Mtakatifu ambao unatuyeyusha kuwa mmoja, sisi ni mmoja katika Kristo, na kwa ajili ya wakati huu wa ushirika kwenye Neno, tunalolikaribia sasa, tena asubuhi ya leo.

⁴ Tunataka kukushukuru kwa yale yaliyokusudiwa kwetu katika juma hili lililopita, kwa ajili ya kukutana na marafiki zetu wapendwa, watoto Wako, na kwa kuhisi hiyo roho nzuri ya upendo na unyofu mioyoni mwao, nasi tunashukuru sana, Bwana, kweli Maandiko ni sahihi, “tutakapokusanyika pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu.”

⁵ Bariki sehemu inayofuata ya ibada. Wabariki ndugu zetu, wachungaji wetu, Ndugu Parker Thomas, mtumishi Wako, Roho Mtakatifu akitenda kazi juu yake na kumsaidia, Bwana, anataka kukutumikia Wewe kwa moyo wake wote. Ninaomba ya kwamba shauku zake zititimizwa, na shauku iliyo nyuma ya kila mkono ulioinuliwa hapa asubuhi ya leo.

⁶ Wabariki watumishi Wako wote kote nchini katika siku hii ya sabato, naomba uwatie mafuta wahudumu Wako kila mahali wanaosimama mimbarani. Jalia wagonjwa waponywe, waliopotea waokolewe, na wale walio tayari, wampokee Roho Mtakatifu. Mungu na aheshimiwe leo kwa sababu ameiacha iwe siku. Katika Jina la Yesu. Amina.

⁷ Mwaweza kuketi. Ninawazia juu ya ule wimbo mkuu wa kale:

Ni tamu sana kumtumaini Yesu,
Kuamini tu Neno Lake;
Kujaribu tu kutegemea ahadi Yake,
Kujua tu, “BWANA ASEMA HIVI.”

⁸ Hii ni . . . Nilikuwa niki mwambia mchungaji wenu wa thamani hapa, Ndugu yetu Parker Thomas, kwamba ninaamini huu umekuwa mmoja wa mikutano yenye matokeo ya kiroho sana ambayo nimekuwa nayo sijui ni lini. Ni—nilishuka, nikasema, “Sasa, ninashuka na usiku wa leo nitasema tu maneno machache, halafu nitawaita watu jukwaani na kuwaomba, wala—wala sitaki kusema mengi kupita kiasi,” mnaona.

⁹ Nikasema, “Sasa, Ndugu Parker ni mwalimu, basi sehemu yangu itafaa nini kule chini?” Na—nawe unakatiliwa mbali tu, unaona, unajua ninalomaanisha, Ndugu. A—anaendelea tu kusonga mbele, Roho Mtakatifu, *kwa hiyo*, na halafu, muda si muda wajua, unaangalia chini na kusema, “Aha, ni karibu saa tatu, nina hakika,” ni karibu saa tano. Kwa hiyo, unaninii tu. . . Vema, tu—tunapenda tu kushiriki kwenye Neno, na tuna furaha sana.

¹⁰ Nami na—najua mmekuwa na wakati mzuri sana shuleni, ama, m—mkutanoni huko maskanini. Mnajua nini, enyi watu? Kama ningaliishi karibu na hapa, ninge—ningekuwa mshiriki wa mahali pale huko juu, ningekuwa, hakika ningekuwa. Ninge—ningekuwa moja kwa moja. . . Mimi ni mshiriki wake; ninamaanisha, ni—ningekuwa nikihudhuria huko, nilikuwa mshiriki wake, kwa sababu nilibatizwa ndani yake. Hiyo ni kweli. Nilibatizwa katika ule—ule ushirika mkuu.

¹¹ Mwajua, ninatoka kwenye ka—kanisa la Kibaptisti, nao Wabaptisti wanaamini ya kwamba wakati unaponinii. . . unabatizwa kwa Roho Mtakatifu unapoamini. Nao pia wanaamini ya kwamba kama unekuwa katika kanisa la Kikristo, ama—ama kanisa lingine lolote, ukibatiza katika namna ile ile ya ubatizo wanaotumia, desturi ile ile, hata hivyo, unapokuwa Mbaptisti, huna budi kubatizwa tena. Kwa maneno mengine, unabatizwa, kwa maji, katika ushirika wa Kibaptisti. Vema, nina furaha tumebatizwa kwa Roho mmoja katika ushirika wa Bwana Yesu, mnaona, huo ndio ubatizo wa kudumu.

¹² Nilipokuwa nikiingia, kulikuwa na ndugu aliyesimama pale nje, alikuwa na kamera ya sinema, naye alikuwa akiimalizia, tukarudi nyuma. Nilidhani mlikuwa mkiimba *Amini Tu*, nami nikaanza kupanda vipandio, ndipo nikamwona ndugu huyu wa thamani, Kitu fulani kikasema tu, “Nenda mahali alipo.”

¹³ Alikuwa akiichukua sinema. Naye alikuwa akinipa ushuhuda, akasema kwanba miaka kumi iliyopita mke wake, akiwa na kansa huko Pennsylvania, katika mmoja wa mikutano yetu, mmoja wa mikutano yetu ya mwanzoni, aliponywa kansa. Naye huyu hapa chini kabisa leo, Ndugu Roe, ninaamini alisema ndilo jina lake.

Huku maskini jamaa huyo mdogo amesimama pale, nywele zake zote zimechanwa, jamaa mdogo mzuri, nami nikasema, “Huyu ni baba yako, ama babu yako?”

Akasema, “La, Bwana.”

Nikasema, “Je, unaishi karibu na hapa?”

¹⁴ Akasema, “Ninatoka Charlotte.” Ninii tu. . .? . . . Ninajua umetoka kusini. Matamshi yake yalimsaliti. Alikuwa ni maskini jamaa mdogo mwenye sura nzuri, maskini mcheshi mdogo tu

mrefu *hivi*, mwajua, wanapendeza, ninawapenda hao jamaa wadogo.

¹⁵ Hapa ndani asubuhi ya leo kuna maskini ndugu yangu Mswidi. Wakati mmoja mimi, bila kumjua, nilimtetea kwa yote yaliyokuwa ndani yangu. Nami nilikuwa ndio kwanza nirudi kutoka Uswidi, naye Ndugu Joseph alikuwa na mvutano mkali huko Chicago, nao walikuwa na mengi dhidi yake, ama, walimkemea kwa sababu tu alitaka kuwa ndugu, na kushirikiana na mtu yeyote aliyeunyosha mkono wake na kusema, “Nipe mkono,” Joseph alikuwa tayari kuishika, kwangu mimi, huyo ni Mkristo. Vema.

¹⁶ Lakini kulikuwa na kundi la wahudumu waliosema, “Yeye anashirikiana na watu *fulani*, amekuwa nao kanisani mwake,” Mvua ya Siku za Masika, na kadhalika. Nasi tulikuwa na mkutano ulioandaliwa huko Chicago, nikasema, “Lakini hivi sisi si tunapaswa kuwa wasio na mipaka ya madhehebu?”

Kasema, “Naam, lakini wangeninii,” jamaa huyu akasema, “wangenifukuza kanisani mwangu kama nikimruhusu aingie.”

¹⁷ Nikasema, “Basi kamwe hatutaenda, kama hawezi kuingia.” Kwa hiyo yeye. . .Nikaruka Chicago kwa sababu hiyo. Nasi tumekuwa marafiki wasiri maishani mwetu mwote. Sasa, kama tungeketi chini na kujaribu kuyajadili Maandiko, huenda tukapitana nusu maili au zaidi, inapofikia kwenye ya Kimaandiko, lakini inapofikia upendano wa ndugu, sisi ni kitu kimoja. Ninajua anampenda Mungu, anaamini jambo lile lile kunihusu mimi, nasi tumekuwa na ushirika kila mahali.

¹⁸ Sasa, anaenda kwenye huduma za kimishenari huko Afrika kutoa . . .kutayarisha mikutano mahali zilipo shule zake kubwa. Maskini jamaa huyo alikuwa, kamwe hafadhiliwi, hadha- . . . hadhaminiwi na mtu yeyote, bali ono moyoni mwake kwenda Afrika, na huko ana maelfu. Alikuwa kwenye kanisa letu huko Jeffersonville, akaonyesha sinema yake ya shule yake, ninataka kuja na kumsaidia.

¹⁹ Basi asubuhi ya leo, nilikuwa nikila kiamshakinywa hapa chini kwa Howard Johnson, nami nikaona baadhi ya marafiki zangu wakipita, basi ni nani aliyeingia, ila Joseph, akaketi chini, na kula kiamshakinywa pamoja nasi. Tukaenda nyumbani, nasi tunaishi karibu sana.

²⁰ Nimefadhaika sana kwa siku chache kwa sababu ya ono, sikuwa nimewaambia watu jambo hilo moja kwa moja, nami, kwa namna fulani nilifadhaika. Nashangaa, “Hiyo inaweza kuwa ni nini? Inawezaje kuwa?” Nilimchukua mke wangu, nasi tukaenda kando, nami nikafanya mazoezi tena, “Ni wapi huko chini barabarani, ambapo mimi . . .? Hivi nimekosa mahali hapo? Imekuwaje?”

²¹ Ndipo kitu Fulani kikasema, wakati sisi . . .alikuwa tu amesimama chumbani mwangu, muda kidogo tu kabla sijafanya

maombi, nije huku. Nami nilikuwa nikitaka kuzungumza asubuhi ya leo, kufundisha juu ya *Mti wa Bibi-arusi*, lakini sauti yangu ilikuwa imeharibika, nami nikasema, “Afadhali niukwepe huo,” maana ni mrefu. Nami nikasema. . . Vema, ni—nilitembea. . . Kitu fulani kikasema, “Mpeleke Joseph huko nje uani.” Nami nikamkumbatia tu, tukatoka nje uani.

²² Tukatembea kupitia kwenye misonobari hii mikubwa, mizuri sana, inaonekana kana kwamba upepo unaovuma kupitia pale unaimba, “Kuna Nchi ng’ambo ya mto,” Nami, nikisimama pale pamoja na maskini rafiki yangu, tukizungumza, na jambo *fulani* nililokuwa nikizungumza naye juu yake, ambalo ni mimi na yeye tu tulijualo, naye akasema, “Lakini, Ndugu Branham, ambapo Bwana alikupa Maandiko haya miaka thelathini iliyopita, lakini je, uliwahi kusoma *hili*, chini yake?” Ilinifanyia jambo fulani, nikamhisi Roho Mtakatifu akishuka tu kote kutuzunguka.

²³ Nikasema, “Asante, Joseph.” Nikamkumbatia, nikarudi mlangoni, nikaingia, nikaichukua Biblia yangu, na hapo ndipo hasa. . . Mbona, sikuwahi kusoma, ila hivyo vifungu vichache tu vya kwanza, sijui. Kwa ajili ya saa hii tu, hivyo tu.

²⁴ Mnajua Yesu aliyachukua Maandiko wakati mmoja, na kusoma tu *kiasi fulani*? Kiasi tu kilichokuwa kitimizwe wakati huo, na kuyaacha mengine, maana sehemu hiyo ilimhusu Yeye wakati huo, na sehemu inayofuata inamhusu Yeye mara ya pili sasa. Huenda nikazungumza juu yake usiku wa leo, Bwana akipenda.

²⁵ Ninataka kwenda, alasiri ya leo, niichukue Biblia yangu niende mwituni peke yangu, maana limenichochea sana ndani sasa. Kamwe sikuwahi kuliwazia, kamwe sikujaribu kulisoma. Ishiri-. . . yapata, vema, yapata miaka thelathini, thelathini na mmoja iliyopita, na kila kitu ambacho Yeye aliniambia kimetimia, na katika miezi sita tu iliyopita sehemu ya mwisho ya hilo ono asubuhi hiyo ilitimia, nayo ilikuwa hii hapa. Kuchanganyikiwa, nadhani, ndivyo ningeliita wakati huo, mnaona, kamwe sikujua tu nielekee wapi, naye Joseph akasema, “Lakini uliwahi kusoma yaliyosalia?” Nayo hiyo hapo, sikujua hilo. Mungu akubariki, Joseph.

²⁶ Naam, ni—ni. . . Ni kwamba, ninawapenda watu wa Mungu, nanyi je? Kitu halisi tu kulihusu. Labda usiku wa leo, Bwana akipenda. . . Ninataka kwenda alasiri ya leo, nione kile atakachoniambia, la kufanya. Ninajisikia vizuri zaidi juu yake sasa, najua hilo. Nilishika tu vifungu viwili ama vitatu, nami nikawazia, “Loo, jamani! Hiyo ni. . . Kwa nini sikusoma hayo? Kwa nini sikuyawazia?” Mnaona? Lakini kamwe sikuliona, sasa, maana wakati haukuwa umewadia.

²⁷ Sasa, Joseph atatuacha aende Afrika kufanya maandalizi kwa ajili ya mikutano. Ndugu Parker Thomas amekuwa mwema

sana kuniomba nirudi tena mwaka ujao, kwenye wakati wa mkutano. Nami ninatumaini ya kwamba hayo yatakuwa ni mapenzi ya Bwana, ninaweza kufanya hivyo, nikutane na kila mtu hapa tena mwaka ujao. Nao ushirika ni mtamu sana.

²⁸ Na sasa, tunataka kutoka hapa kabla ya adhuhuri, na, ili mweze kula, na kupumzika, na kadhalika, na kurudi tena jioni hii. Je, mna ibada ya jioni, ama ibada ya alasiri, Ndugu? [Ndugu Parker Thomas anasema, “Nafikiri, labda, tutakuwa na ibada ya ubatizo alasiri ya leo, Ndugu Branham.”—Mh.] Sasa, mtu yeyote anayetaka kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo . . . Huo utakuwa wapi? Kanisani mwako? [“La. Utakuwa nyuma ya nyumba yangu, kwenye ziwa. Kuna ziwa huko nyuma.”]

²⁹ Loo, haya basi! “Haya hapa maji. Ni kitu gani kinachotuzuia?” Vema. Ninyi nyote matowashi shukeni sasa mkaingie majini. Na kama hujapata ubatizo wa Kikristo bado, kwa kuzamishwa, njoo nyumbani kwa Ndugu Parker Thomas, parokia alasiri ya leo, na kutakuwa na maji kwa ajili ya ibada ya ubatizo.

³⁰ Na huo ni wakati mzuri wa kulitatua mara moja milele. Hiyo ni kweli. “Kwa maana aaminiye *na* kubatizwa ataokoka.” Hiyo ni kweli? “Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi *mtapokea* kipawa cha Roho Mtakatifu.” Kama hiyo si kweli, basi sijui kilicho kweli.

³¹ Paulo aliwaambia hao watu katika Matendo, mlango wa 19, Paulo, akipitia kwenye pwani za juu za Efeso, anakutana na wanafunzi fulani, mhubiri mashuhuri wa Kibaptisti kule juu alikuwa akihubiri, akithibitisha kwa Biblia ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo, akasema, “Hivi . . .?”

³² Paulo akapitia, na Akila na Prisila, watengeneza mahema, marafiki wa Paulo, ambao kabisa, Akila na Prisila walikuwa wachungaji wa hilo kanisa. Yeye, Akila alikuwa ndiye mchungaji wa hilo kanisa, kanisa la kwanza huko Rumi. Ndipo wakati Klaudia alipokuwa amewafukuza Wayahudi wote, alirudi Palestina. Ningependa kuzungumza na kanisa Katoliki juu ya hilo. Naam, bwana. Kuhusu, kwa nini—kwa nini Petro alikuwa kule wakati huo? Vema. Sasa, lakini alikuwa amefukuzwa kutoka Rumi, na alikuwa ameletwa kwenye nchi ya uenyeji wake, maana . . .

³³ Ndipo Akila na Prisila, ndipo waliporudi, kisha kukawa na maaskofu wa Kirumi kule walioingiza mafundisho yote ya sharti, nao hao ndio waliolanzisha kanisa lenu la kwanza la Katoliki, papo hapo.

³⁴ Ndipo yeye akaanzisha kanisa Katoliki la pili, ambalo basi wakati Paulo alipokuja Rumi, alikuja kwenye kanisa la pili. Nataka mtu fulani anionyeshe mahali ambapo Paulo alipata kwenda kwenye kanisa la kwanza, asingeamini hayo mafundisho ya sharti. Je, ungeweza kuwazia Petro, Myahudi, aliyefundisha

dhidi ya sanamu, akiweka sanamu kanisani? Je, mnamkumbuka Petro, mkali sana kwenye Neno, huku akidumu na Neno? Hivi angeweza kamwe kukubali mafundisho ya sharti? Nafikiri: La, la, si—si huyo, huo ni upumbavu tu. Lakini hilo hapo linaenda, na hivyo ndivyo lilivyoanza.

³⁵ Sasa, tunaona ya kwamba Paulo, akipitia kwenye pwani ya juu ya Efeso, ndipo akawakuta wanafunzi fulani, walikuwa wakishangilia, wenye furaha, akawaambia, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?” Je, hilo si lilikuwa ni pigo la kushindwa kabisa kwa Wabaptisti? Mnaona? Mbaptisti alisema unampokea Roho Mtakatifu *unapoamini*, na hivyo ndivyo hasa yule mwanzilishi wao wa kwanza alivyofikiria. Hivyo ndivyo Apolo, alisema, naye alidhani walikuwa tayari, kila kitu kilikuwa sawa. Akasema. . . Walikuwa wakipaza sauti, wakiwa na wakati mzuri sana, Paulo akasema, “Hilo ni sawa.”

³⁶ Akila na Prisila walikuwa tayari wamewaambia, “Tuna maskini kasisi mmoja, Paulo. Lakini atakapokuja, atawafundisha Neno la Mungu kwa udhahiri zaidi.”

³⁷ Kwa hiyo akapitia pwani ya juu, naye akakutana na mwanatheolojia huyu wa Kibaptisti, mtu mashuhuri, mtu mwema, naye akaliambia kusanyiko lake, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Wakasema, “Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu.”

Akasema, “Basi mlibatizwaje?”

Wakasema, “Loo, tumebatizwa.”

“Vipi? Kwa kitu gani?”

Kasema, “Kwa ubatizo wa Yohana.”

Akasema, “Yeye alibatiza tu kwa toba,” ile Dhabihu haikuwa imechinjwa bado, mnaona, “sio kwa ondoleo la dhambi.”

³⁸ Hiyo ni kweli. Matendo 2:38 ilisema, “Tubuni, mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi.” Mnaona?

³⁹ Lakini akasema—akasema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Kasema, “Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu yeyote.”

Kasema, “Mlibatizwaje?” Hauna budi kuwa ni muhimu.

Naye akasema, “Hatujui hata kidogo kama kuna Roho Mtakatifu.”

Akasema, “Mlibatizwaje, ama, kwa kitu gani?” Ile ya asili inasema “kwa vipi?”

Naye akasema, “Kwa ubatizo wa Yohana.”

⁴⁰ Akasema, “Yohana kweli alibatiza kwa ajili ya toba, akiwaambia watu, wanapaswa kumwamini Yeye atakayekuwa, yaani, Yesu Kristo.” Nao waliposikia haya, wakabatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo. Paulo akaweka mikono yake juu

yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu, akaja juu yao; nao wakanena kwa lugha na kutabiri. Hiyo ni kweli. Vema. Loo, hilo ni Fundisho zuri la Kipentekoste kwangu. Ndivyo hakika.

Vema. Kwa hiyo sasa, kama hujapata ubatizo wa Kikristo, shuka uje alasiri ya leo.

⁴¹ Halafu basi hapa si muda mrefu uliopita, kabla tu hatujaanza, mnajua ya kwamba maskini mama yangu wa thamani ndiyo kwanza aipitie barabara hiyo. Na kama ningalikuwa na wakati, ningewaambia jinsi ilivyotukia, jinsi Bwana alivyoniambia, nikaachana na safari ya kuwinda niliyokuwa nayo, nikatumwa mahali pengine, na kuniambia kile ningepata, kisha nirudi, na mahali hasa kila kitu kilikuwa kimewekwa, kikamilifu.

⁴² Nililiambia kanisa kabla sijaondoka, nikasema, “Nitamwua dubu wa futi tisa mwenye rangi ya fedha. Nitamwua kuro ambaye pembe zake zina urefu wa inchi arobaini na mbili kutoka chini kwenda juu, naye atakuwa amelala kwenye mandhari ndogo.” Sijawahi kuwa humo nchini. Nikaliambia kanisa. Sehemu ya hilo kanisa imeketi hapa, asubuhi ya leo. Hiyo ni kweli, enyi Kanisa? Inua mkono wako, unayetoka kwenye Maskani ya Branham.

⁴³ Nilisema hasa mahali atakapokuwa. Baadhi ya ndugu waliambatana nami wapate kujua, tulienda katika nchi fulani, ambayo sijawahi kuiona hapo awali, na mahali penyewe hasa, ambapo kila kitu kilikuwa. Yule—yule dubu mkubwa mkali wa fedha ana urefu wa futi tisa kutoka ncha hadi ncha, na ninii . . . aliuawa mahali pale pale Yeye aliposema.

⁴⁴ Yule kuro, amelala, akiniangalia moja kwa moja chini ya mlima. Ndipo yule kiongozi akasema, “Ndugu Branham, kama hizo, pembe za kuro, zina urefu wa inchi arobaini na mbili, nitazimia.”

⁴⁵ Nikasema, “Afadhali uanguke chini, kwa sababu zitakuwa.” Wakati alipotoa *utepe* wake, basi hizo hapo kwenye alama papo hapo, hazipiti kwa moja juu ya kumi na sita, inchi arobaini na mbili kabisa. Nikasema, “Hivi huamini?”

⁴⁶ Yeye, mwaka mmoja kabla ya hapo tulikuwa tumerudi mahali fulani, naye alikuwa tu ni mwongofu mchanga, naye akasikia kuhusu hiyo mikutano. Mke wake ni mwaminio wa Kipentekoste. Yeye ni kiongozi, Ndugu Southwick, juu . . . Akasema, “Mtu akiwahi kuhoji hilo, na waandike na kuniuliza mimi.” Akasema, “Acheni niwasimulie.” Anaishi huko nyuma kabisa, hiyo ni nchi ya jua la usiku wa manane huko Yukon. Kwa hiyo yeye . . .

⁴⁷ Nasi tulikuwa tumerudi, nao Wahindi huko nyuma, walikuwa—walikuwa wameyavuka yale maji, nayo ma—maji yalikuwa yametukatilia mbali, wala tusingeweza kurudi. Kwa

hiyo tuliketi tu pale siku chache, tukizungumza tu, tukiangalia mambo makuu porini na kupiga picha za vitu mbalimbali.

⁴⁸ Na kwa hiyo, akaendelea, Eddie akaendelea kumwambia mmoja wa wahudumu kuhusu maono, naye akasema, “Loo, jamani! Laiti ningaliweza tu, laiti ningaliweza kumleta ndugu yangu huko chini!” Naye akasema, “Ndugu yangu amekuwa na kifafa, ndugu yangu mdogo,” kasema, “amekuwa na kifafa tangu alipokuwa na umri wa yapaya miaka mitatu, hushikwa na kifafa mara nne ama tano kwa siku.” Kwa hiyo nilijua alikuwa—alikuwa akimwomba Mungu, bali siwezi kuyafanya maono yatokee, hayo hutokea tu; hiyo ni neema ya Mungu. Si—sininii. . . Kwa hiyo tulikuwa huko nyuma. Nilimwomba mara mbili au tatu, huku yeye hajui. Kesho yake tukazunguka. . .

⁴⁹ Tulikuwa na farasi wapatao ishirini na mmoja, na—na huko chini kwenye hizo safari, kwa kawaida, niliwafunga mkia kwa hatamu, namna *hiyo*, lakini katika milima hiyo huwezi kuitumia namna hiyo kwa sababu utapoteza msururu wote wa farasi, na wakati mwingine wangeanguka kutoka kwenye jabali.

⁵⁰ Nasi tulipokuwa njiani tukitoka, tuliwaachilia hao farasi, hawa farasi wachanga hubingirisha mizigo yao na kadhalika. Nilikuwa nikipanda farasi sana, na baba yangu alikuwa mpanda farasi.

⁵¹ Na kwa hiyo tulikuwa tunakuja nami nilikuwa huko nyuma nikihangaika, Bud alikuwa mbele, huyu Ndugu Eddie, mimi na Ndugu Bud, na Mkristo mwingine aliyeitwa Chris Berg. Na kwa hiyo, Bud alikuwa amepanda farasi, mbele huku farasi wa mtangulizi akijaribu ku—kuongoza, nami nilikuwa nikija nyuma, mimi na Eddie, tukiwatoa farasi hao kwenye kinamasi. Na—nadhani nyote mnajua kinamasi ni nini. Nao wangeingia humo, ni kama mchanga didimizi.

⁵² Tulikuwa na kadhaa huko chini, na, loo, nilikuwa matope kutoka kichwani hadi miguuni, na—na kule nikiwatoa hao farasi. Ndipo mmoja wao akaruka ndani, nami nilikuwa. . . Nikaruka ndani juu yake, nikainua kichwa chake juu namna *hiyo*, tukamfungia kamba, tukaitupa kwenye pembe ya matandiko yangu namna *hiyo*, kisha tukamchukua farasi mmoja, na kuondosha mizigo hiyo mingine, tukamtoa mle. Ndipo unachukua tu matope, na kujikwangua namna *hiyo*.

⁵³ Na, loo, loo, jamani, hao farasi wachanga, huwezi, wanaenda tu njia yoyote, wana umri wa miaka miwili au mitatu, ndio kwanza wafunzwe, wala wao si farasi wa safari za mbugani.

⁵⁴ Na kwa hiyo, tulikuwa tukitoka, nami nilikuwa nimeamka, na nilikuwa nimepanda kwenye matandiko, na—na—na Eddie alikuwa pale. Ndipo ilitokea niliangalia kwenye hiyo misonobari mikubwa mno ya kupendeza, theluji upande wa juu. Mungu, jalia niishi kule katika, kama kuna Utawala wa Miaka Elfu unaokuja, jalia niishi humo.

55 Hiyo ni... Mnaweza kuwa na vitalu vyenu vyote vya kupendeza, viliyopunwa vilivyo, na majengo yenu makubwa, na mitende yenu yote ya Miami iliyoangaziwa, na yote mtakayo, lakini hebu niwe nayo jinsi tu Mungu alivyoituma, katika asili yake tu, ninaipenda tu namna hiyo. Loo, ninaweza tu kusimama juu ya vilima hivyo, niende kuwinda, na kupanda juu kabisa kwenye kilele cha vilima na kuketi pale, na kuinua tu mikono yangu na kulia. Niangalie upande wa pili pale, niwazie, “Mungu, hapana shaka hivyo ndivyo unavyoipenda, hivyo ndivyo hapana shaka Wewe, hivyo ndivyo ulivyoifanya. Kwa nini imbidi mwanadamu kuichafua, kuifanya kitu kingine, kuipotosha?”

56 “Siku moja,” nikawazia, “Bwana, nijalie nitembe kwenye vijia vyako vikubwa vya wanyama visivyo na kikomo.” Natumaini nitakutana nanyi ndugu wawindaji wote kule chini, hasa, mahali nilipokuwa nikitazama. Ninatazamia jambo hilo. Bila shaka mnajua hayo ndiyo maombi ya Mhindi kutoka... wakati...

57 Nikishuka kwenda kule, nilikuwa nikiangalia upande wa pili namna hiyo, ndipo nikamwona maskini jamaa huyo katika ono. Yule farasi alisimama mwenyewe, haikunibidi kumsimamisha. Ndipo nikaangalia ono hilo kwa dakika chache, na wakati liliponiacha, nikaona lilikuwa kwa ajili ya ndugu yake Bud. Nilikuwa na farasi mmoja tu wa mbio, nikamchochea maskini farasi wangu, na kumgeuza, nikaenda kasi sana kwa Eddie. Nilikuwa na farasi mmoja aliyekimbilia kichakani pale, ndipo ni—nikasema, “Eddie. Eddie, Ndugu.”

Akasema, “Kuna nini, Ndugu Branham? Unaonekana mweupe kama shuka.”

Nikasema, “Nina BWANA ASEMA HIVI.”

“Ni kitu gani? Kwa ndugu yake Bud?”

58 Nikasema, “Naam.” Nikasema, “Endelea kuwasukuma farasi mbele.” Nami nikamchochea farasi wangu, nikavuka, na kupitia kwenye kile kinamasi na kadhalika, yapata dakika kumi na tano nilikuwa huko mbele, mbele ya ule msururu, nikamwendesha farasi karibu na Bud, na kuweka mkono wangu nyuma ya tandiko lake, kisha nikasema, “Bud.”

Akasema, “Naam, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Nina BWANA ASEMA HIVI.”

Akasema, “Unamaanisha nini?”

59 Nikasema, “Kwa siku mbili ama tatu zilizopita, tangu tumerudi hapa, daima umezungumza kuhusu, kama ungeweza kumleta ndugu yako katika mmoja wa ile mikutano.”

60 Akasema, “Naam, Ndugu Branham.” Naye ananinii tu, ye—yeye hata hakuwa amempokea Roho Mtakatifu bado,

amempokea sasa, bali hakuwa amempokea wakati huo. Naye akasema, “Mimi . . . Naam, hiyo ni kweli.”

Nami nikasema, “Ndugu yako . . .” Nikatoa wasifu wake.

Akasema, “Hiyo ni kweli kabisa, hiyo ndiyo sura yake.”

⁶¹ Nikasema, “Wala hili halitatendeka kwa mtu mwingine, bali litatendeka kwa ndugu yako.” Nikamwambia la kufanya, nikasema, “Tuma mtu akamwite ndugu yako, amlete hapa.” Ilikuwa kwenye barabara kuu ya Alaska, aliishi mahali pa kale ambapo Wamarekani kule, ambapo wengi wao walikufa katika kujenga hiyo barabara. Nayo serikali yote ikaangukia humo. Naye alikuwa akiongoza, ana maili mia sita mraba mle ndani, yeye ni kiongozi mwenye leseni. Na kwa hiyo, akasema . . . Nchi isiyostaarabika sana, nzuri sana ya kuwindia.

⁶² Ndipo nikasema, “Bud, angalia, wakati mvulana huyo atakapokuja, naye ashikwe na kifafa tena, nyakua shati lake, na useme, ‘Ndugu Branham aliniambia nifanye hivi katika Jina la Bwana,’ na kulitupa hilo kwenye tanuru.” Nikasema, “Kifafa kitamwacha. Unaniamini mimi?”

Akasema, “Kwa moyo wangu wote.”

⁶³ Akaagizia na kumleta ndugu yake, akamleta kule juu, halafu asubuhi hiyo akaenda kutengeneza vijia. Maskini mke wake, maskini Mkristo mzuri, lakini yeye . . . Akawa mkali, angeshikwa na pupa pia. Kwa hiyo hivi, hakuwa ameondoka nyumbani kwa zaidi ya kama dakika thelathini huko chini mahali fulani, naye akashikwa na kimoja cha vipindi hiyo vya kifafa. Kwa kawaida, maskini mke huyo angerukia dirishani, chochote kile, akimtoroka, lakini wakati alipomwona akibingirika na kugaagaa, huku ibilisi huyo akimfanyia hivyo, ilitokea akakumbuka. Naye aliniamini.

⁶⁴ Huyu hapa anamjia, na kumtagaa, maskini mwanamke huyo mdogo juu ya mtu huyo mkubwa mno, mwenye mabega mapana, akamtagaa, na kulinyakua shati hilo upesi, akaelekea kwenye tanuru hiyo, machozi yake yakitiririka mashavuni mwake, kasema, “Mungu mpendwa, Ndugu Branham alitwambia tufanye jambo hili, nami nalitupa hili mle ndani, katika Jina la Yesu Kristo.” Hajawahi kuwa na kifafa tangu wakati huo na kuendelea.

⁶⁵ Nilipomwambia kuhusu hayo maono, na yale yangetukia, tukishuka mlimani, tulimpiga risasi huyo kuro mlimani, akasema, “Ndugu Branham, kulingana na ono hilo,” tulikuwa katika kuvumwani ya kuro, mwajua, ambako unaweza kuona kwa maili na maili, wala hakuna kitu, kuvumwani tu ya manjano, akasema, “kulingana na yale uliyoniambia, sasa, mtu huyo atakayekuwa ameava li—lile shati,” Eddie kule chini, lile shati lenye mirabamiraba, “utamwua dubu mkubwa mkali wa rangi ya fedha mwenye urefu wa futi tisa?”

Nikasema, “Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.”

⁶⁶ Akasema, “Ndugu Branham, si—si—silitilii shaka neno lako, Ndugu. Ningewezaje kutilia shaka neno lako?” Kasema, “Lakini angalia, ninaweza kuona kila chembe ya ardhi wala hakuna kitu, hakuna kichaka kirefu *hivyo*, hakuna kitu ila kuvumwani za kuro. Huyu dubu yuko wapi?”

Nikasema, “Yeye ni Yehova-Yire, ‘Bwana atajipatia Mwenyewe.’” Nikasema, “Je, umewahi kusikia ile hadithi kuhusu wale kuchakulo wakati ule?”

Akasema, “Eddie aliniambia habari zake.”

Nami nikasema, “Vema, Yeye angali ni Mungu. Kama akisema atakuwako . . .”

⁶⁷ Akasema, “Vema, Ndugu Branham, kama Mungu amekwambia hilo, na huyu kuro alikuwa amelala hasa . . . Mbona, sijapata kuona mmoja kama huyo,” akasema, “sioni jinsi ulivyowahi kumpata, hapa, katika yadi hamsini kutoka kwake.” Kisha kasema, “Vile hasa ulivyosema.” Kasema, “Uliniambia,” kasema, “ndugu yangu aliponywa hakika kabisa.” Kasema, “Hiyo imekuwa ni zaidi ya mwaka mmoja uliopita, alikuwa anashikwa na kifafa mara tatu ama mara nne kwa siku, hajawahi kushikwa na kimoja tangu wakati huo.” Akasema, “Ningewezaje kutilia shaka?” “Lakini,” kasema, “Ndugu Branham, nimeishi katika milima hii maishani mwangu mwote, wala sijawahi kuona mwenye rangi ya fedha maishani mwangu.” Kasema, “Nimemwona dubu wa kawaida, lakini si mwenye ncha za fedha.” Hiyo ni aina adimu.

⁶⁸ Nikasema, “Lakini kuna mmoja hapa.” Kwa hiyo nikakitwaa kichwa, pembe za huyu, nasi tungezibeba, nilikuwa na bunduki, nasi tungepokezana, tukishuka, ikitubidi kwenda *hivi* tukishuka kilimani, hiyo kuvumwani ya kuro. Jamani, ilikuwa yapata maili tatu na nusu kushuka moja kwa moja kabla hata hujafika msituni. Na kwa hiyo, mnaona, hiyo hata si nchi ya dubu, hiyo ni ya kuro.

⁶⁹ Kwa hiyo tukashuka hatua kwa hatua. Tulibadilisha . . . Hiyo nyara niliyobeba ilikuwa na uzito wa . . . Vema, huyo kuro mwenyewe alikuwa na uzito wa karibu mia tisa, lakini ilitubidi kuiacha nyama pale, nami nikachukua tu juba, nazo hizo pembe peke yake zilikuwa na uzito wa ratili mia moja na hamsini. Kwa hiyo mimi huyu hapa nikijaribu kuzivuruta chini ya kilima, namna *hii*, juu ya mabega yangu.

⁷⁰ Ndipo tulipofika karibu yapata . . . Tulifika kwenye mto mdogo wa barafu, naye akasema, “Wazia hilo, Ndugu Branham, tuko tu yapata maili moja kufikia ambapo . . . Ninaweza kuona kwa macho yangu ya kawaida ambapo hao farasi wamesimama, nami ninaona kila kilima, ati nawe utamwua dubu wa kijivu mwenye ncha za fedha akiwa na urefu wa futi tisa?”

Nikasema, “Hiyo ni kulingana na Neno la Mungu lililoniambia yapata miezi mitatu iliyopita, wala halijawahi kushindwa kamwe.” Nikasema, “Unashuku hilo, Bud.”

Akasema, “Kunradhi, Ndugu Branham. Sishuku.” Kasema, “Moyo wangu ni ninii sana... Kamwe si—siwezi kulielewa.” Kasema, “Yuko wapi huyo dubu?”

Nikasema, “Sijui.” Nikasema, “Mungu amemweka hapa mahali fulani.”

Akasema, “Wazia jambo hilo, dubu ambaye sijawahi kumwona, na yule ambaye Mungu alikwambia...” Kasema, “Huyo ni Mungu yeye yule aliyekwambia habari za ndugu yangu.”

Nikasema, “Kweli kabisa.”

Kasema, “Ndugu Branham, tia risasi kwenye bunduki yako.”

Nikasema—nikasema, “Nitakuwa na wakati wa kufanya hivyo.”

⁷¹ Tunashuka kilimani. Tunafikia yapata—yapata nusu maili, naye alikuwa amebeba, nami nilikuwa na bunduki. Kwa hiyo tukaketi chini, tukipumzika, akasema, “Ndugu Branham, wazia tu, tuko nusu maili tu.”

⁷² Nikasema, “Bud!” Nami nikasema, “Atakuweko, usijali.” Ndipo nikaangalia, nikasema, “Bud, ni kitu gani *kile* kinachosimama *kule* juu, yapata maili mbili huko juu, kilele cha mlima?”

⁷³ Akavaa darubini, kasema, “Ndugu Branham,” ilionekana kama ng’ombe wa maziwa, akasema, “ni dubu mkubwa mkali, masalaale! Basi mwangalie huyo, mawimbi meupe ya kijivu yakivuma kwenye kutua kwa jua alasiri ya leo, yeye ni wa kijivu. Kamwe sijapata kumwona awali.”

Nikasema, “Tunangojea nini?”

Akasema, “Ninaamini kama ungempiga risasi tu kutoka hapa, ni umbali wa maili mbili, utampata.”

Nikasema, “Lakini Bud, kulingana na ono, nilikuwa tu karibu sana naye.”

⁷⁴ Tumechoka sana, tumedhoofika, nasi tulikuwa tumetembea angalau maili ishirini siku hiyo juu ya milima hiyo, kwa hiyo basi, tukaanza kupanda, kurudi juu tena. Ndipo nikafika yapata yadi mia tano, naye Bud akasema, “Ndugu Branham,” akasema, “uliwahi kumpiga risasi dubu wa fedha hapo awali?”

Nikasema, “Nimewaua dubu wengi, lakini sijawahi kumwua dubu wa fedha.”

Naye akasema, “Hao ndio wakali kuliko wote.” Kasema, “Hawajui kufa.”

Nikasema, “Hakuna dubu ajuaye kufa.”

Kwa hiyo nikasema... Akasema, “Lakini Bwana alikupa huyo, sivyo?”

Nikasema, “Loo, naam.”

⁷⁵ Kwa hiyo nilikuwa na .270 ndogo, ni bunduki ndogo. Na kwa hiyo, basi, nikapanda juu kidogo zaidi, naye akasema, “Ndugu Branham, hivi huoni afadhali umpige risasi kutoka hapa? Afadhali tusimkaribie sana.”

Nikasema, “Ono lilisema tulikuwa karibu sana naye.”

⁷⁶ Kwa hiyo tukaingia kwenye korongo lingine dogo, tukapanda, na tulipofanya hivyo, pale, jamani, yeye ameketi tu yapata yadi mia mbili na hamsini pale, ningeweza kuona meno yake makubwa, ya manjano yakiuma chini namna *hiyo*. Alionekana kama lundo kubwa la nyasi kavu, inchi kumi na nane katikati ya masikio. Na—naye alikuwa mkubwa mno, mguu yapata upana *huo*, na makucha, mwajua, naye ameketi tu pale. Loo, alionekana mwenye sura nzuri kweli, na katili.

Kwa hiyo Bud akasema, “*Ahem*,” akasema, “Ndugu Branham, hebu nikwambie mahali pa kumpiga risasi.”

Nikasema, “Naam, Ndugu?”

Akasema, “Mgongoni, unaona,” kasema, “ndipo hawawezi kusimama basi, unaona.”

Nikasema, “Lakini lile ono lilisema, ‘Mpite risasi moyoni.’”

Akasema, “Basi afadhali ufanye hivyo.”

⁷⁷ Risasi ya kwanza ikampata. Na hapo tukashuka, akasema, “Ndugu Branham,” tulikuwa tumebeba hizo pembe, hatukuwa na utepe wa kupimia, akasema, “hizo pembe zinaonekana kama tisini.”

⁷⁸ Nikasema, “La, ni arobaini na mbili tu.” Akasema... Nami nikamwambia Eddie, nikasema, “Sasa, angalia, yule mvulana mdogo ataweka mikono yake papo hapo kupima.”

⁷⁹ Basi tulipofika mahali ambapo wale farasi walikuwa... Tusingeweza kumleta huyo dubu, ilitubidi kurudi kesho yake. Wala huwezi kumleta dubu... Whiu! Huwezi kumleta farasi karibu na dubu mkubwa mkali, unajua hilo, harufu yake, huyo ametoroka. Tukakata kamba mbili ama tatu tukijaribu kumtoa nje. Na kwa hiyo basi, loo, walikuwa na vikapu vimetandaa juu ya kila kitu, matandiko ya farasi, yalikuwa yametawanyika, hao farasi walimwogopa sana huyo dubu mkubwa mkali, harufu yao.

Kwa hiyo tukaendelea kushuka, ndipo tuliposimama, hao wavulana walikuwa pale wakingojea, Eddie na mwanawe, naye akasema, “Ninataka kuzipima hizo pembe.”

⁸⁰ Nikamwendea Eddie, nikasema, “Eddie, angalia mvulana huyo akiweka mikono yake chini ya hizo pembe sasa, kama nilivyowaambia kabla hatujafika hapa.” Kwa hiyo anashuka, anatoka kwenye... utepe kutoka kwenye ninii yake... maskini

utepe wake wa kupimia. Maskini mvulana huyo akakaribia, akaweka mikono yake juu yake.

⁸¹ Eddie akasema, “Asifiwe!” Kweli kabisa. Akainuka moja kwa moja namna *hiyo*, akawa tu mweupe usoni, akasema, “Ndugu Branham,” kasema, “angalia hapa, haizidi kwa moja juu ya kumi na sita, inchi arobaini na mbili kamili.” Yesu hashindwi kamwe.

Akasema, “Ndugu Branham, nitakuwa wapi mwaka mmoja tangu leo?”

⁸² Nikasema, “Sasa, Bud, wewe ni mwongofu mchanga tu kwa Kristo, sijui mahali utakapokuwa.” Nikasema, “Ninaweza tu kusema jinsi Yeye anavyoniambia, hayo ndiyo nisemayo, na hayo tu ndiyo niyuayo.” Unaona? “Sijui.”

⁸³ Sasa, ninarudi katika nchi fulani, mpate kujua, nitakaporudi mwaka ujao, nitampata dubu wa hudhurungi aliye karibu mara mbili ya ukubwa huo. Mtaona kama ni kweli ama si kweli. Nilimwona. Tulipokuwa tumesimama, nikaweka mikono yangu juu ya mapaja yake huku amelala chini, namna *hiyo*, nami ningeweza kuweka mkono wangu kwenye nyonga zake namna *hiyo*, naye amelala chini. Sasa, mtaona kwamba hiyo ni kweli ama si kweli.

⁸⁴ Kuna mengi sana kuhusu hilo. Lakini ilitokea tu niliwazia, ninapaswa kuwa nikifundisha shule ya Jumapili. Mnaona? Loo, marafiki, nyote mnaona maono haya madogo hapa? Si ajabu ninyi ndugu wahudumu wakati mwingine mnashuku, “Vema, huenda ikawa ni telepathia ya kiakili. Huenda ikawa ni saikolojia.” Hebu mnionyeshe mahali pengine linapoendelea. Vipi kuhusu hawa wanasaikolojia mashuhuri, wanatelepathia? Wao hubahatisha, wakati mwingine linatendeka, wakati mwingine halitendeki, na ni *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*. Lakini Mungu ni mkamilifu wala kamwe hashindwi.

⁸⁵ Ni nini mmoja wa ninii...? Mpiga ramli ni nini? Ni mtumishi wa Kristo aliyepotoshwa. Kosa lolote ni nini? Ni *haki* iliyopotoshwa. Kweli kabisa. Kamwe hakuna... Ni mara kwa mara tu, ndivyo hivyo, kuubahatisha Ukristo. Usibahatisha, hakikisha kwamba uko sahihi. Pata... Kufa tu kwa nafsi yako na uzaliwe mara ya pili na Roho wa Mungu ndipo utajua. Ndipo hakuna... *kama zote*, na *na zimeondoka* kwake.

Nampenda, Nampenda (Utukufu!)
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

⁸⁶ Nilimwona mtu fulani, mtu aliyeambatana nami. Kamwe sikumtambua akiwa pale, bado, najua, Ndugu Fred Sothmann. Ameketi *pale*, naye alienda Dawson pamoja nami. Hiyo ni kweli, Ndugu Fred Sothmann? Huyo *hapo*. Nilichora ile picha kwenye kioo changu cha mbele cha gari jinsi hasa (Hiyo ni kweli?), kabla

halijatendeka. Loo, hilo limetukia...Ni wangapi wanaojua, wanaosafiri? Kwa wageni hapa. Naenda zangu barabarani, naye Bwana atasema mambo mbalimbali yatakayotukia, nayo yatakuwa vivyo hivyo hasa, kote kote. Hakika ndivyo ilivyo. Mnaona? Ninii tu...[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda—Mh.*] Hivi hamumpendi? Uimbeni tu.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Juu . . .

⁸⁷ Hakuna kubahatisha tena, tuko ndani ya Safina, ulimwengu umefungiwa nje, tuko ndani ya Yesu sasa. Loo, ushirika!

⁸⁸ Sasa, Mungu, tusaidie kuwa na ushirika kwenye Neno Lako. Ninapolisoma, Bwana, ninajua ya kwamba Maneno Yako hayatashindwa, yangu hushindwa, mimi ni mwanadamu tu, sisi sote ni wanadamu tu. “Mwanadamu ni kitu gani hata umkumbuke? ama Mwana wa Adamu kwamba Wewe umwangelie?”

⁸⁹ Hakika, Bwana, hatuna kitu tunachoweza kutoa, kwa sababu tulipewa hapo mwanzo. Tusingeweza kuwa hapa kama si kwa ajili Yako. Na kuwazia ya kwamba neema ya Mungu imeshuka katikati yetu katika siku hizi za mwisho. Naye Mungu, yule Muumba mkuu, amejitambulisha Mwenyewe kwetu kwa kutusamehe dhambi yetu, na kuonekana mbele zetu katika njia za ajabu sana, kama alivyoahidi ingekuwa wakati wa jioni. Nuru za jioni zinaangaza. Tujalie, Baba, kwamba tutashirikiana kwenye Neno Lako sasa. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁹⁰ Samahani kwa kuwashikilia namna hiyo. Hebu na tusome sasa Maandiko, mafupi tu. Tutatoka sasa, katika yapata dakika thelathini na tano, arobaini, Bwana akipenda.

⁹¹ Hesabu 14 . . . Nilisema hivyo kwa sababu huenda nikakosea. Mimi—mimi . . . Mnaona, mimi sijui atakalofanya, mtu fulani anaweza kupata kitu fulani hapa katika dakika chache, Roho Mtakatifu huenda akaingia katika hili, ninatazamia jambo fulani kutukia, sijui. Kwa hiyo mimi—mimi . . . kama sijui, basi nitasema tu, “Kama ni mapenzi Yake,” Mnaona? Naam, bwana.

⁹² Ninajua nini? Roho Mtakatifu huenda akaja hapa juu, na kumgusa mmoja wa hawa ndugu wanaoketi mimbarani, na huenda akafanya jambo fulani hapa kugeuza tu kitu hicho chote. Huenda kukawa na kushuka kwa Roho Mtakatifu katika dakika chache, na huu—huu usingefungwa kwa majuma mawili au matatu zaidi, mchana na usiku tu, ukiendelea daima, ninii yote . . . Sijui atakalofanya. Na, mwajua, tena, huenda tukasikia Baragumu ikilia.

⁹³ Hesabu 14:41 hadi 45, tukisoma Neno la Bwana sasa:

Basi Musa akasema, Kwa nini ninyi sasa kuyahalifu maagizo ya BWANA? lakini halitafanikiwa jambo hilo.

Msikwee, kwa kuwa BWANA hamo kati yenu; msije mkapigwa. . . mbele ya adui zenu.

Kwa kuwa Waamaleki na Wakanaani wako kule mbele yenu, nanyi mtaanguka kwa upanga: kwa sababu mmerudi nyuma msimwandame BWANA, kwa hiyo BWANA hatakuwa pamoja nanyi.

Lakini walithubutu kukwea mlimani hata kileleni: ila sanduku la agano la BWANA halikutoka humo maragoni, wala Musa, hakutoka.

Ndipo basi Waamaleki, na Wakanaani waliokaa humo mlimani, wakatelemka, wakawapiga, na kawaangusha, hata kufikilia Horma.

⁹⁴ Sasa, kwa ninii tu, kutoa somo dogo kutoka hapa, asubuhi ya leo, kuzungumza tu. Sasa, ninaamini ya kwamba tuko hapa kuninii, katika shule ya Jumapili kufundishwa, kujifunza. Na kama tunaweza kurudi nyuma na kuona katika Agano la Kale, na katika Agano Jipya, jinsi watu walivyobarikiwa na Mungu, na jinsi walivyolaaniwa na Mungu, na tuone kile Mungu alichoheshimu na alichohitaji, ndipo tutakuwa na wazo fulani la jinsi ya kudumisha baraka za Mungu. Hivi hamwoni hivyo?

⁹⁵ Sasa, sitahubiri, sina sauti ya kutosha kwa ajili ya jambo hilo, lakini mimi. . . Basi kumbukeni, daima, tumekuwa tukiendelea mpaka Septemba hii ijayo. Nina yapata siku mbili kati ya hiyo mikutano hadi Septemba, Bwana akipenda.

⁹⁶ Sasa, tunataka kujua, hebu niliseme tena sasa, tuchukue muda wetu kwa dakika hizi chache tulizo nazo, sasa, hatuna budi kurudi nyuma, na kama tunaweza kuona kile Mungu alichotaka, kile alichohitaji, kile alicholaani, kile alichobariki, basi hebu na tuyachukue kama mifano.

⁹⁷ Ninaamini katika Waebrania mlango wa 11, la, mlango wa 12, alisema, “Kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila dhambi, au, kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu.”

⁹⁸ Sasa, hatuna budi kurudi. Paulo hapa, kwa kuwa tunaamini yeye alikuwa ndiye mwandishi wa Waebrania, alikuwa akionyesha vile watu wa imani na mashujaa hodari walivyokuwa, ndipo tunaweza kuchukua upande huo mwingine. Nina kitabu nyumbani kinachosimulia maneno ya mwisho, Ndugu Nugent, nilikipata kutoka kwake miaka mingi iliyopita, maneno ya mwisho ya wanaume na wanawake mashuhuri walioishi duniani. Nami ninaamini ilikuwa ni Mary aliyelowa Damu, huko Uingereza, ambaye maneno yake ya mwisho, wakati alipokuwa akifa alisema, “Ningetoa ufalme wangu, nipate dakika tano zaidi za maisha.”

⁹⁹ Nina maneno ya mwisho ya Abraham Lincoln. Nina maneno ya mwisho ya Stonewall Jackson. Mnajua maneno ya mwisho ya Jackson yalikuwa nini, yule jemadari mkuu wa kusini? Ninaungana nanyi waasi katika kumshukuru Mungu kwa ajili ya jemadari kama Jackson, hajawahi kulinganishwa mahali popote na jemadari mwingine yeyote, ni juavyo, nionavyo mimi. Alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu, naye Jackson alisema, alipokuwa akifa, alikuwa akijiandaa kuvuka ule mto, akasema, “Hivi karibuni tuta uvuka ule mto, kisha tutaketi chini ya ule mti na kupumzika.” Hiyo ni kweli.

¹⁰⁰ Nilisikia maneno ya mwisho ya Dwight Moody, alisimama, na kusema, “Ati hii ni mauti?” Kasema, “Hii ndiyo siku yangu ya kupewa ukuu.”

Na maisha ya watu mashuhuri yote
hutukumbusha
Tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu; (Ninapenda hilo.)
Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
Huku akisafiri kwenye bahari adhimu ya
maisha,
Ndugu mpweke ambaye chombo
kimemwendea mrama,
Akiziona, atatiwa moyo tena.

¹⁰¹ Paul Rader. Ni wangapi waliopata kusikia habari za Paul Rader, hata hivyo? Nilikuwa nikimsikia akihubiri nilipokuwa mvulana mdogo, sikujua wakati huo kwamba ninge ueneza wimbo wake, *Amini Tu*, kote ulimwenguni. Wakati Paul alipokuwa akifa huko nje, walialika maskini kundi la waimbaji wanne kutoka kwenye Shule ya Biblia ya Moody. Mnajua yale Paul aliyomwambia rafiki yangu? Wakati alipojua alikuwa yuafa, alikuwa na kansa, akasema, “Laiti ningaliuchukua ujumbe wangu wa neema na kuupandikiza kwa hawa Wapentekoste motomoto, badala ya kuja hapa,” hilo ndilo lililomwua, kasema, “ningekuwa afadhali zaidi.”

¹⁰² Kwa hiyo Moody. . . Paul alikuwa na ucheshi. Yeye na Ndugu Bosworth, na hao wote, walikuwa tu marafiki wasiri, Billy Sunday. Ndugu Bosworth alikuwa na mkutano huko juu pamoja na, wakati mmoja huko Chicago, Maskani ya Rader, na kwa hiyo, Billy Sunday alikuwa huko majuma matatu, naye alikuwa amehubiri mahubiri yake yote. Naye, Paul alikuwa huko yapata miaka miwili, naye alikuwa akiendelea kuhubiri. Kwa hiyo Billy akamwambia Paul, akasema, “Paul, ni wakati gani ambapo wewe huishiwa na mahubiri?”

Akasema, “Nitakapopata pindokombo katika bomba.”

¹⁰³ Na kama mtu yeyote alipata kumsikia Paul akihubiri, angeanzia katika Mwanzo, na kuishia katika Ufunuo, a—

angeihubiri Biblia nzima kila wakati anapohubiri. Nilikuwa nikimwangalia, angechukua ninii, kitu fulani niani mwake, angerudi nyuma kabisa, mtu mkubwa mno, angevuta suruali yake juu, mwajua, naye huyu hapa anakuja mbio upesi alivyoweza, na karibu asimame juu ya mimbara, kama dubu mkubwa huku amenyoosha mikono yake.

¹⁰⁴ Lakini alipokuwa akifa huko nje, Shule ya Biblia ya Moody ilituma kundi la waimbaji wanne, nao walikuwa wamesimama pale huku mapazia yote yamefungwa hospitalini, wakiimba, *Karibu Na Wewe Mungu Wangu*. Paul akainuka, akasema, “Aisee, kwani ni nani anayekufa, mimi au nyie?” Akasema, “Yafungueni hayo mapazia, mniimbie nyimbo nzuri za Inji-... nyimbo changamfu za Injili.” Amina. Kwa hiyo wakaanza kuimba:

Huko chini msalabani ambapo Mwokozi
wangu alifia,
Huko chini kwa ajili ya kutakaswa na dhambi
nililia;
Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Loo, utukufu kwa Jina Lake!

¹⁰⁵ Akasema, “Yu wapi Luke?” Huyo ni ndugu yake, wengi wenu mlimjua Luke, aliondoka hivi majuzi tu. Luke na Paul walikuwa ndugu wawili waliokaa pamoja, kitu kama mimi na Billy, mwanangu.

¹⁰⁶ Kasema, “Yu wapi Luke?” Luke alikuwa kwenye chumba cha pili, hakutaka kumwona ndugu yake akifa. Kasema, “Mwambieni tu Luke aje huku.” Wakamwingiza Luke ndani, Luke akijaribu kujizuia kuangua kilio. Paul akainuka, akaushika mkono wake, akasema, “Luke, tumepitia vita vingi pamoja, sivyo, Ndugu?”

Akasema, “Naam, Paul.”

Akasema, “Wazia hilo, katika dakika tano kuanzia sasa, nitakuwa nimesimama Mbele za Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake.”

Maisha ya watu mashuhuri yote
hutukumbusha
Ya kwamba tunaweza kuyafanya maisha yetu
adhimu,
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu.

¹⁰⁷ Hebu niondoke namna hiyo. Hebu niondoke na ushuhuda huo, kama aliokuwa nao Moody. Hebu niondoke na ushuhuda kama aliokuwa nao Paul, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza. Mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi.”

¹⁰⁸ Kwa hiyo, nikirudi nyuma katika Agano la Kale, nilikata kauli hizi kwa ajili ya ujumbe mdogo sasa: *Kudhania*. Webster, nimeliandika hapa, Webster inasema *kudhania* ni “kuthubutu bila mamlaka halisi.” Huku ndiko *kudhania*. Ama, katika mabano ameandika, Webster, “kulichukulia kijuu juu,” kulichukulia tu kijuu juu, au “kuthubutu bila mamlaka,” ama “kuchukulia jambo fulani kijuu juu tu.”

¹⁰⁹ Sasa, hilo ni jambo ambalo Kanisa halipaswi kufanya. Hu—huna hakika nafsini mwako ikiwa unadhania tu, kwa kuwa unalichukulia tu vivi hivi. Sasa, tuna, kila mwaka tunapita likizo. Ninii, ninasikitika kusema jambo hili, lakini inaonyesha hata hivyo, Mkristo wa kawaida wa Marekani, *anavyojiita* . . . Billy Graham alitoa tamshi lili hili wakati mmoja, kama ulisoma makala yake kuhusu ni walevi wangapi waliokuwa katika ule *unaoitwa* Ukristo. Yule *anayejiita* Mkristo wa kawaida wa kanisa fulani, na mwenye dhambi vile vile, ambao kwangu mimi wote wako katika hali ile ile, watu hunywa pombe na kujaribu kufunika dhambi zilizopita, udanganyifu, kusema uongo, na mwishoni mwa juma, wanajaribu kulewa. Wanawazia tu, “Vema, nitaupita tu.”

¹¹⁰ Wanadhania ya kwamba hiyo ndiyo njia sahihi ya kufanya hilo. Wanajisikia ya kwamba hiyo ndiyo njia ya kusahau dhambi zako, kuzinywea tu pombe, hutambui unalundika tu dhambi zaidi. Lakini wanadhania ya kwamba hiyo ndiyo njia ya Marekani ya kufanya jambo hilo, na hiyo huenda ikawa ni kweli, bali siyo njia ya Biblia ya kulifanya. Lakini wanadhania ya kwamba hilo ni sawa. Nilisema hilo kwa . . .

¹¹¹ Hapa si muda mrefu uliopita nilikuwa nikizungumza juu ya somo ambapo nilikuwa huko Canada pamoja na Ndugu yangu mwema Sothmann *pale*, nami nikashuka kwenye ho—hoteli kubwa mno ambayo alikuwa mkarimu sana kuniweka mle. Nao Wamarekani walikuwa huko juu Canada, klabu *fulani* ya Marekani, walikuwa wakifanyia mkutano wao mkuu mle.

¹¹² Nami nawaambia, nilipoingia usiku huo, vema, kulikuwa na “Bi Marekani,” pamoja na . . . Loo, balaa! Huku chupa za wiski zimejaa kila kitu. Ndipo nikapanda kwenda chumbani, nikatoka, nami nikamwangalia maskini jamaa huyo, kulikuwa na watu kadhaa waliotoka, wanaume wameshikana, klabu fulani, basi wakati mimi . . . maskini lifti hiyo, nikasema, “Jamani! Whiu!”

Akasema, “Loo, wana wakati mzuri sana.”

Nikasema, “Hakika wanaonekana hivyo.”

¹¹³ Kwa hiyo tukaenda hadi mlangoni, nami nikafungua mlango, na tulitoka tu kwenye lifti, na tukaanza kushuka, na palikuwa na wasichana wawili, wote wawili wakiwa wamevaa pete za arusi, maskini wanawake warembo, wamevaa tu nguo zao za ndani, wamesimama mwishoni mwa ukumbi. Nao

walikuwa na chupa ya wiski mkononi mwao, na walipoanza kushuka kupitia pale, wakijaribu kushikana, macho yao yalikuwa baridi, yamekodolewa, huku rangi midomoni mwao imechujuka, na kitu hicho cheusi. Nao hao wanawake wakiweka pete hiyo kwenye. . .

¹¹⁴ Unaonekana kama tumbili, si mwanadamu, namna hiyo. Kuna shida gani? Mnaona? Na upuuzi huo wote, na huo mtindo mkubwa wa kukata nywele kichwa-maji, mwajua. Wewe ni mrembo, usijifanye uonekane kama mnyama wa zamani za kale. Unaona? Pendezwa tu na jinsi Mungu alivyokuumba.

¹¹⁵ Nao hawa hapa, wasichana hawa, wanawake, wamesimama pale nao wakaanza kushuka ukumbini, wakiyumbayumba, ndipo baadhi ya wanaume wakatokea, walevi, wakamshika mmoja karibu na mahali fulani mwilini mwake hakupaswa kupashika, na kujaribu kumshika, naye, huku akiyumbayumba, angeshuka kuja, naye angewakwepa makundi kadhaa yao. Nilirudi tu nyuma na kuliangalia.

¹¹⁶ Basi walipokaribia, huku wamesimama pale wakiwa na vazi dogo tu la ndani, bila shaka hizo ni zaidi ya wanazovaa baadhi yao, halafu walikuwa na chupa hii, mmoja wao akampa mwingine kinywaji, na huyu mwingine akanywa mdomo mzima kutoka kwenye chupa hii ya wiski, naye akavuta sketi hii ndogo juu kadiri alivyoweza, akarusha miguu yake juu sana, na kupaza sauti “Whoopie!” Akasema, “Huku ndiko kuishi! Haya ndiyo maisha.”

¹¹⁷ Niliviangalia vidole vyote viwili, nikawaza, “Labda mume yuko nyumbani akimlea mtoto.” Ni kitu gani? Wakijaribu kuwa na raha kidogo, kile wanachoita “raha safi ya Marekani.” Walikuwa wakiosha vyombo, wakifanya kazi ofisini, nao wanainii tu—kwa namna fulani tu, kama nilivyosema jana usiku, wakijaribu kutoa presha.

Nami nikasema, “Samahani! Hayo si maisha, hayo ni mauti.”

Kwa hiyo akaangalia kote, akasema, “Unataka kinywaji kutoka kwenye chupa yangu?”

¹¹⁸ Nikamshika mkono, nikasema, “Mimi ni mhubiri wa Injili, mimi ni Mmarekani pia, lakini ninakuonea aibu!” Ndipo huyo mwingine akaanza kutoroka, nikamshika kwa mkono mwingine, nikasema, “Je, ninyi wanawake huenda kanisani?” Nao wakaonekana kutoa ulevi kidogo.

Akaishusha hiyo chupa, kasema, “Naam, Bwana.” Mmoja wao alikuwa ni mwalimu wa shule ya Jumapili.

Nikasema, “Hivi hujionei aibu, kujiita Mkristo?”

¹¹⁹ Nikajaribu kuwashikilia, walikuwa wakivuta, na kushtusha, wakirukaruka tu namna *hiyo*, nao hao wakashuka ukumbini. Mmoja wao akaanguka na kujibwaga sakafuni, naye huyo mwingine akajaribu kumwinua akitanguliza miguu, ndiyo

tamasha mbaya kuliko zote ulizowahi kuona. Nikawaza, “Mungu, waweza je kuangalia mambo kama hayo?”

¹²⁰ Lakini wanadhani hilo ni sawa, kwa sababu wao ni washiriki tu wa madhehebu fulani, kama wanalizaliwa mara ya pili wasingekuwa wakifanya hivyo.

¹²¹ Ninaamini ilikuwa ni Calvin, la, ilikuwa ni John Smith, sina hakika sasa, huyo mtu, lakini siku moja katika misheni yake, mmoja wa watakatifu wakuu wa mwanzoni wa miaka mia mbili ama mia tatu iliyopita, ninasahau alikuwa ni nani, ninaamini ilikuwa ni Mmethodisti, John Smith, huenda alikuwa ndiye, lakini, hata hivyo, walikuwa wamesimama mlangoni, naye huyu hapa mlevi akaja barabarani, naye akaanguka kwenye mfereji wa maji machafu. Ndipo kulikuwa na mtu aliyepitia hapo akasema, “John, huyo hapo mmoja wa waongofu wako.”

¹²² Akasema, “Naam, hiyo ni kweli. Kama alikuwa ni wa Bwana, asingekuwa hapo.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hivyo ndivyo. Kama umeongoka kwa kanuni ya imani, kama umeongoka ukawa wa madhehebu, kama umeongoka ukawa wa kanisa, utafanya mambo hayo, lakini unapokuwa mwongofu wa Kristo, umezaliwa mara ya pili, nawe umekufa kwa mambo hayo, na u hai. Lakini watu wanaendelea moja kwa moja wakidhani ni sawa kufanya hivyo, wakithubutu bila mamlaka.

¹²³ Wahubiri, watu wazuri, watu wema, wanahubiri fundisho la kimadhehebu wakidhani hilo tu ndilo linalohitajika (Na huku Biblia hii inasema, “Yeyote atakayeondoa Neno moja Kwake, au kuongeza neno moja Kwake, huyo ataondolewa katika Kitabu cha Uzima kwa ajili yake.”), akisema, “Humhitaji Roho Mtakatifu siku hizi, huyo alikuwa ni kwa ajili ya siku zilizopita.” Kwa nini? Hawawezi kufundisha jambo lolote tofauti, wakifanya hivyo, wanatengwa.

¹²⁴ Wanasema, “Hakuna kitu kama uponyaji, Roho Mtakatifu alitolewa tu kwa mitume.” Sasa, wanapata hilo kwa sababu wamefundishwa hilo shuleni mwao, wakidhani kwamba hilo ni kweli, bali ni kosa. Mbingu na nchi zitapita, bali Neno la Mungu halitapita. Naye akasema, “Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu Kweli,” lakini wao wanadhani ya kwamba hilo ni sawa.

¹²⁵ Wanasema, “Vema, hayo tu ndiyo wanayojua.” Kama ulishuka kwenda kwenye mkahawa kwa ajili ya chakula chako cha kutwa, na . . . nadhani bado ni *chakula cha kutwa* hapa, huko ninakotoka, huko Indiana, wanajaribu kupata Marekani ya kisasa, wanajaribu kusema, “Tuna kiamshakinywa, na tuna chakula cha mchana, na *cha kutwa*.” Sikuzote nimeachwa nje. Chakula changu cha jioni kinaingilia wapi? Mnaona? Mnaona? Ninasema, “Je, mnakula *chakula cha kutwa* cha Bwana, ama *chakula cha jioni* cha Bwana?” Upuuzi. “Kujigamba,” hivyo tu.

¹²⁶ “Loo, yeye ni msomi, ameelimika,” wakidhani hilo ni sawa, hatuhitaji hilo. Wakihubiri fundisho la kimadhehebu wakidhani

ya kwamba hilo ni sawa, nao watu wanaenda kujiunga na kitu hicho, wakidhani hilo ni sawa, hilo tu ndilo wanalopaswa kufanya, kudhania tu, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa.”

¹²⁷ Mwajua, siku moja nilikuwa kwenye mstari wa maombi, na nikiendelea kuja, ndipo palikuwa na mama mmoja aliyekuja jukwaani, na vema, ana haki ya kufanya lolote atakalo, nadhani, naye alikuwa na vito vya kutosha kumdamini mmishenari mara kumi kote ulimwenguni. Nami nikasema, “Wewe ni—wewe ni Mkristo?”

Akasema, “Mimi ni Mmarekani, si hilo latosha?”

¹²⁸ Nikasema, “Si kwangu mimi, halitoshi.” Nikasema, “Nilikuuliza kama wewe ulikuwa ni Mkristo,” um-hum, sio mwomba lifti, la, la, bali Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Alifikiri kwa sababu alikuwa ni Mmarekani hilo lilitosha. Mnaona?

¹²⁹ Ndugu Bosworth alikuwa na mstari wa maombi huko Detroit wakati mmoja, ndipo msichana mmoja akaja jukwaani kuombewa, akasema, “Je, wewe ni Mkristo?”

Mbona, alishtuka sana, akasema, “Nataka uelewe, mimi huwasha mshumaa kila usiku!” Wakidhania, hilo tu ndilo linalowabidi kufanya.

¹³⁰ Hao ni watu wenye mioyo minyofu, wao ni wanaume na wanawake, nao, moyoni mwao wa—wa—wanataka kumtumikia Mungu. Hao watawa wanaingia kwenye nyumba za watawa, wahudumu wanaenda kwenye seminari, wanapata digrii za saikolojia, na jinsi ya kuinama mbele za watu, na jinsi ya kuwa, na matokeo ya kisaikolojia hilo liliyo nayo kwa watu, wakidhania ya kwamba hilo tu ndilo linalowabidi kufanya, hata katika baadhi ya madhehebu yetu makuu, ya Kipentekoste, sasa sizungumzi juu ya Wamethodisti, na Wabaptisti, ninazungumza juu ya Wapentekoste.

¹³¹ Hapa si muda mrefu uliopita walipata matatizo fulani. Kila mmoja alijitenga kwa masuala madogo, wakidhani hilo ndilo walilopaswa kufanya; hilo ndilo ambalo hawakupaswa kufanya. Ninyi kaeni pamoja, ninyi nyote, msipeleke mambo yenu nje namna hiyo, yaleteni hapa na kuyaombea. Kama unaweza kuwa na suala lako na bado unampenda ndugu yako, vema. Lakini unapoteza heshima na ushirika na ndugu yako, suala lako limekuua. Sawa.

¹³² Lakini haya basi. Wanadhani ya kwamba hilo tu ndilo linalowabidi kufanya, kwa sababu hilo ndilo wanalofundishwa, wanaenda tu kujiunga na kanisa. Wanasema, “Wewe ni Mkristo?”

“Mimi ni Mmethodisti.”

“Wewe ni Mkristo?”

“Mimi ni Mpresbiteri.” Na halafu wanajiunga na hilo.

Na sasa unasema, “Je, wewe ni mwaminio?”

“Mimi ni Mpentekoste.”

¹³³ Sasa, hebu ninyoshe hilo kwa ajili yenu, hakuna kitu kama dhehebu la Kipentekoste. Pentekoste ni tukio, si dhehebu, Wakatoliki wanayo, Wabaptisti wanayo, Wapresbiteri wanayo, mtu yeyote anaweza kuwa Nayoy. Ni tukio, si... Huwezi kuliundia dhehebu. Ukiwa na dhehebu lako, umeondoka kwenye Pentekoste basi. Unaona? Kamwe hawakuunda dhehebu. Mungu hajawahi kuwa na dhehebu, hata wakati mmoja.

¹³⁴ Ninawapa changamoto mnionyeshe na ninampa changamoto mwanahistoria yeyote kuniambia, na kunionyesha katika historia wakati wowote ambapo Mungu alituma ujumbe, nao wakauundia dhehebu; lilikufa papo hapo, wala halikufufuka tena, ni kitu kilicholaaniwa. Kwa hiyo angalieni tu nyuma katika historia yenu mwone kama hiyo ni kweli. Lakini wanaunda kanuni zao za imani na kujiunga nazo, watu wanafikiri hilo ni sawa.

¹³⁵ Enyi wanawake, mwajua, ninawapenda, dada yangu, unajua hilo, sisimami nipate kuwaudhi, ninawapenda, lakini nitafanya nini Kule kwenye Siku ile, wakati nikijua Biblia inafundisha yale wanawake wanapaswa kufanya? Halafu basi, ninajua kwamba ni kweli. Ndipo basi, kama mlinzi akiketi ukutani na kumwona adui miongoni mwa watu, wala asiwaonye, Mungu alisema, “Nitaitaka hiyo damu mkononi mwa huyo mlinzi.”

¹³⁶ Wachungaji wanapowaruhusu kukata nywele zenu, na kusema ya kwamba hiyo ni sawa, mchungaji huyo anakwambia jambo ambalo si kweli. Anapokuacha uvae nguo isiyo ya staha, na kukwambia ya kwamba—ya kwamba hilo ni sawa, hilo ni kosa. Wala sio... Wewe—wewe ni mrembo.

¹³⁷ Unajua, kila kitu mle ndani, katika ukoo wa kike na wa kiume, sikuzote wa kiume ndiye mrembo kuliko wote. Chukua jogoo na tembe, chukua jamii ya ndege. Mchukue kulungu, fahali au jike? Mchukue paa, dume au jike?

¹³⁸ Kila kitu sikuzote ni kirembo sana katika ukoo wa kiume, isipokuwa kwa jamii ya binadamu, wa kiume ana sura mbaya, mnene, mwenye ndevu usoni mwake, mara nyingi ana upara na anaonekana wa kuparua, amejaa nywele. Lakini mwanamke ni mtanashati, mrembo; hapo ndipo Shetani alipo, papo hapo. Hapo ndipo alipochagua katika Edeni, hapo ndipo alipopitia huko Edeni, huyo ndiye amemtumia tangu wakati huo. Na hebu niambieni taifa lolote katika historia, baadhi yenu watoto wa shule, katika kuanguka kwa taifa, mara umama ulipovunjika pamoja na uwanawake, uti wa mgongo wa taifa hilo ulivunjika.

¹³⁹ Nena kuhusu maadili katika nchi yetu, nina kijipande kutoka kwenye gazeti kwenye Associated Press, ambapo wavulana wetu walipoenda ng'ambo, kwamba wanne kati ya kila sita walitalikiwa na mke wao aliyebaki nyumbani, kabla

hawajakaa huko miezi sita. Pia kulikuwa na watoto haramu wengi zaidi waliozaliwa katika Jimbo la New York mnamo, katika mwaka mmoja kabla ya hivyo vita, kuliko askari waliouawa katika miaka yote minne ya vita; wakidhani hilo ni sawa.

¹⁴⁰ Wanawake wanavaa nguo ndogo, za kizinifu, na kutembea mtaani, wanasema, “Naam, mimi ni Mkristo.” Wanadhania hilo ndilo jambo wanalopaswa kufanya. Sasa, tafadhali, Dada, mimi ni ndugu yako, kama mama yako alikuwa mwanamke anayefaa, angekwambia vivyo hivyo, ama baba yako, ama mume wako.

¹⁴¹ Na mwanamume yeyote, atakayemwacha mke wake atoke nje mtaani amevaa kaptura na vitu kama hivyo, inaonyesha ni *mwanamume* kiasi gani ndani yake. Kumwachilia mkewe aketi pale na kuvuta sigara mbele zake, huku anajua kwamba kitu hicho. . . Je, watoto wake watakuwa nini?

¹⁴² Msihofie kuhusu ukomunisti kutupiga, tayari tumejipiga wenyewe, ni maadili yetu wenyewe yaliyooza. Yalianzia wapi? Kwa sababu Injili ililegezwa mimbarani, ndicho chanzo chake, wahubiri dondoadume, wasio na ubatizo halisi wa kutosha wa Roho Mtakatifu nafsini mwao kusimama na kulitangaza Neno la Mungu. Usimcharaze mtoto kwa ajili ya kutowajibika kwa vijana, wacharaze wazazi, ni kutowajibika kwa wazazi, wanaacha waendeleo nako.

¹⁴³ Na hiyo ndiyo sababu ninawakemea sana hao makasisi huko. Mnawezaje kusoma Biblia ile ile niisomayo? Vivyo hivyo na wale manabii mia nne huko chini katika Israeli walisoma Biblia ile ile ambayo Mikaya alisoma, lakini alikuwa tayari, bila woga, kuchukua msimamo wake.

¹⁴⁴ Amosi, katika siku zake, yule nabii jasiri wa Mungu, alienda kule Samaria, akaangalia juu ya mji huo, na kuona huo upotovu wote uliokuwa ndani yake, naye akasema, “Mungu yeye yule mnayedai kwamba mnampenda atawaangamiza.” Aliona upotovu wake.

¹⁴⁵ Walikuwa wakidhani walikuwa sawa, walikuwa na makuhani wao, masinagogi yao, waliwazia, “Mradi mimi ni Myahudi, nimetahiriwa, hivyo tu ndivyo ninavyohitaji kuwa.” Walidai kwamba walimtumikia Mungu. Na wao—wao. . . Walikuwa wamefanya nini? Walikuwa wamechukua mitindo ya mataifa ya nje, walikuwa wamefanya mapatano nao, nao walidhani mradi walipendwa na mataifa ya nje, vema, hilo tu ndilo walilopaswa kufanya. Walifanya mapatano, wakawavua nguo wanawake wao, wakatembea mtaani, wakafanya vichekesho, na chochote kile.

¹⁴⁶ Naye nabii huyo mzee amesimama pale, na macho yake yamejifinya juu ya ndevu zake, watalii walikuja kutoka kote ulimwenguni kuona Samaria hii mashuhuri, lakini nabii huyo aliiona kwa jicho tofauti.

147 Siku hizi watu na wahudumu wanaliangalia Kanisa kama idadi na idadi, bali Mkristo aliyezaliwa mara ya pili huliangalia kwa jicho tofauti, yeye huliangalia kupitia Neno la Mungu, naye anaukemea upotovu ulio ndani Yake. Mungu yeye yule wanayedai kumtumikia atashusha Hukumu juu yao. Unabii wake, ilichukua tu miaka kumi na mitatu kutimia. Jerome wa pili, ni . . . mnaajua jinsi ilivyotukia, Yeroboamu, hasa, ninaamini ndiye. Haya basi, ukajiunga.

148 Dada, kabla sijaliacha, hivi uliwahi kutambua, unapovalia namna hiyo na kutoka nje mtaani. . . Huenda ukawa msichana mdogo, naamini ndivyo ulivyo, kipenzi. Hiyo ni kweli. Ninaamini wewe ni msichana mdogo, siamini wewe ni mbaya, siamini unataka kuwa mbaya. Siamini m—mtawa Mkatoloki wa kike huingia kwenye nyumba ya watawa apate kuwa mbaya. Maskini mwanamke huyo huingia humo kwa sababu anataka kumkaribia Mungu zaidi, siamini wanataka kuwa wabaya. Siamini ya kwamba ungekuwa msichana mbaya, siamini ungemkosea adabu mume wako.

149 Lakini hivi unatambua. . . Yule mtawa Mkatoliki hatambui ya kwamba mfumo unaomtuma kule, wala huitambui roho ya siku hizi, inayokufanya ufanye mambo hayo, unadhani ni sawa, bali sivyo.

150 Sasa, angalia, Yesu alisema, “Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Sasa, unatoka nje umevalia namna hiyo, umevaa hizo kaptura, na umevalia kizinifu kwelikweli, na kadhalika, hakika, wewe ni mrembo, bali Mungu hakukufanya hivyo, Shetani anakufanya chambo, wala hujui.

151 Sasa, hebu mwanamume akuangalie, maskini msichana Mkristo unayeshuka kuja barabarani, kijitoto kizuri cha kuvutia, kisicho na hatia, kimevalia kizinifu kwelikweli, naye mwenye dhambi anakitazama kwa kukitamani, kwenye Siku ya Hukumu, mtu huyu atakapowajibika kwa kufanya uzinzi, ni nani aliye na hatia? Msichana. Mnaona ninalomaanisha? Mimi—mimi. . . Labda siku moja mtaona kwamba si mimi ninayekaribu kujifanya mjuaji. Ni kwa upendo wa kiungu. Mnaona? Nawapenda. Sitaki muwe hivyo.

152 Msiwe kama walimwengu wengine. Ninyi wanawake wa Kipentekoste, dhehebu lenu ndilo lililoalikwa liingie, nao wakajiundia dhehebu. Nao wanajaribu kulinganisha kusanyiko lao na watu waliovalia vizuri, waliojipamba, na waliovalia nadhifu zaidi, huyo ni ibilisi. Msiamini hilo. Wanadhani ni sawa, bali sivyo, Mungu alisema tusifanye hivyo. “Endelea, lihubiri, jiunge,” wanafikiri ni sawa, wakidhanja tu.

Nanyi mwajua, watu wamesema hivi: “Mungu ni Mungu mwema.”

153 “Loo, Ndugu Branham,” mtu fulani aliniambia, “wewe hujaribu kudumu moja kwa moja na Neno hilo, kile tu lisemacho. Hivi hufikiri kwamba haileti tofauti yoyote?”

154 Jamaa fulani alikuwa amenyunyiziwa si muda mrefu uliopita. Naye akasema... Nilimbatiza, na kwa hiyo mtu mwingine akamfuatilia kuhusu hilo, akasema, “Vema, alikuwa tayari amebatizwa.”

Nikasema, “La, hakubatizwa, alinyunyiziwa.” *Kubatiza, baptizo*, linamaanisha “funika, zika.” Nami nikasema, “Mimi nilimbatiza.”

Naye akasema, “Ndugu Branham, wewe ni mkali.”

Nikasema, “Labda ndivyo nilivyo, bali ni kwa sababu nzuri.” Nami nikasema, “Nina bidii kwa Mungu na Neno Lake, nina bidii kwa Kanisa Lake.”

155 Nilikuwa mtu aliyetengwa na jamii, hakuna mtu aliyenipenda wala kunjali, nilipokutana nanyi Wapentekoste mlionipenda, na kuiamini Injili hii, nilikuja miongoni mwenu sio niwe adui kwenu, bali kuwa ndugu kwenu ku—ku—kuwaonyesha Neno la Mungu. Hebu baadhi ya wachungaji waje wasimame karibu nami wakati mmoja, mbele zenu, na waseme ni kosa, hiyo ndiyo njia pekee ya kuthibitisha jambo hilo. Mnaona?

Sasa, hili ndilo lililotukia: nikasema, “Nilimbatiza tena.”

Akasema, “Ndugu Branham, kweli unafikiri inaleta tofauti?”

156 Nikasema, “Ileta kwa Paulo, akasema, ‘Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?’ Wao wakasema, ‘Sisi, hatujui kama Yupo.’ Akasema, ‘Mlibatizwa kwa ubatizo gani?’ Kasema, ‘Kwa Yohana.’ Kasema, ‘Hiyo ilikuwa tu, kwa toba, si kwa ondoleo la dhambi.’ Walibatizwa tena.

157 “Ndipo Paulo akasema katika Wagalatia 1:8, ‘Tkiwa Malaika kutoka Mbinguni,’” sembuse mhubiri, “‘kama Malaika kutoka Mbinguni, angawahubiri Injili nyingine yoyote isipokuwa hii niliyowahubiri, na alaaniwe.’” Hiyo ni kweli. Sasa, unaona, hudhanii. Huna budi kuninii. . . Haina budi kuwa ni kweli, dumu nayo. Lakini kudhanian tu!

158 Wao. . . Mnasikia mengi sana siku hizi, nasema tena, kuhusu Mungu kuwa Mungu mwema. Kulikuwako na mvulana tineja aliyesema si muda mrefu uliopita, kasema, “Unajua, Bwana ananipenda sana, Yeye huniacha tu nifanye lolote.” Jamani!

159 Marafiki, Yeye ni Mungu mwema, nitakubali hilo, bali Yeye ni Mungu wa haki, Yeye ni Mungu anayetaka haki. Anawezaje kuwa mwenye haki na—na asitii sheria Zake Mwenyewe? Anawezaje kuchafua sheria Zake Mwenyewe takatifu? Kama Yeye ni mwenye haki, hana budi kushikilia yale aliyosema. Kama atataka hili kwako, wala usiifikie hatua hiyo, kama Yeye si

mwenye haki, basi kwa nini hakumruhusu Hawa apite na huo upotovu mdogo wa Neno?

¹⁶⁰ Kwa nini akaachilia ile miaka elfu sita ya mateso, na—na—na hatari, na mauti, na huzuni kuipiga jamii ya binadamu? Asingeweza kufanya lingine lolote ila hilo, Yeye ni mwenye haki, na Yeye ni Mungu wa hasira, na Mungu wa haki, na utakatifu Wake, ni . . . kuwa, inampasa Yeye kuwa hivyo, si yodi moja, liko moja kwa moja mstarini, unakuja kwenye hilo, ama uko upande *huu* au upande *ule*. Haidhuru wewe ni mzuri jinsi gani, jinsi ulivyo mpole, jinsi ulivyo mtulivu, jinsi ulivyo mwema.

¹⁶¹ Ni nani anayeweza kuwa mpole zaidi, na zaidi, kile wanachoita upendo, kuliko Sayansi ya Kikristo? Huo ndio msimamo wao wote, ni upendo. Huo sio upendo halisi, hata wanakana Yesu kuwa ni Mungu, wanakana mauti, kuzaliwa, ku—kuzaliwa na bikira, kukana Damu Yake, na kuzungumza tu juu ya upendo.

¹⁶² Ungeweza kuniwazia mimi, nikiwa na mvulana mdogo nikisema, “Loo, Mpenzi, endelea tu. Kama unataka kunywa pombe hiyo, ewe mvulana mdogo mwenye umri wa miaka sita, endelea, Baba hatakuzuia, ninakupenda kupita kiasi. Loo, Mpenzi, kama ukitaka kuchukua bunduki yangu yenye risasi mbili ndani yake, na kifyatua risasi kimewekwa tayari, endelea, ninakupenda sana siwezi kukuzuia.” Huo si upendo.

¹⁶³ Vipi kama alikuwa huko nje mtaani, kasema, “Baba, ninataka kutengeneza mikate ya matope hapa nje,” ambapo magari yanaenda maili sitini kwa saa barabarani?

¹⁶⁴ “Ninakupenda kupita kiasi, Mpenzi, siwezi kukuzuia. Unataka kufanya hivyo, najua hilo. Baba anakupenda sana hata hawezi kukuzuia, nenda huko nje ukauawe.” Baba halisi atamchuna ngozi.

¹⁶⁵ Hiyo ndiyo shida siku hizi, mnajaribu kuhubiri Injili mkiwa mmevaa glavu nyororo, mkidhani ni sawa. Kile Kanisa linachohitaji leo, ni kukemewa vikali. Kurudi kwenye Injili. Unadhani ni sawa, “Mimi ni Mpentekoste, mimi ni *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*. Hilo ni sawa.” Si sawa, si kulingana na Neno. Huna budi kuja kwenye Neno.

¹⁶⁶ “Mungu mwema sana.” Hawadhani ya kwamba Yeye ni Mungu wa haki. Yeye ni Mungu ambaye hana budi kulitimiza Neno Lake.

¹⁶⁷ Sasa, Israeli hapa walidhani ya kwamba walikuwa sawa. Sasa, nina dakika kumi kumalizia, tupate kutoka kwa wakati unaofaa. Israeli hapa walidhani, walipanda juu, Biblia ilisema walifanya hivyo, “Mbona,” wakasema, “angalieni, sisi ni watu wa Mungu. Mungu alishuka kule Misri, na kutuchukua, akamtuma nabii Wake kule chini akiwa na Nguzo ya Moto juu yake, akatuleta kule juu, na kumwua Farao moja kwa moja mbele zetu, akaipiga nchi kwa mapigo, viroboto, chawa,

akatuma moto na mvua ya mawe juu ya nchi. Naye akatulinda. Utukufu kwa Mungu! Haleluya!

168 “Nasi tukaja hapa kwenye Bahari ya Shamu, huyu hapa Farao akaja, Mungu aliifungua tu Bahari ya Shamu kwa nguvu Zake kuu, nasi tukatembea kupitia Bahari ya Shamu. Mungu alitupenda sana akageuka, kasema, ‘Mwangalieni adui yenu pande zote, nitawazamisha nyuma yenu.’ Utukufu kwa Mungu! Isitoshe, bali alitulisha chakula cha Malaika, kilianguka kutoka Mbinguni kila usiku.”

169 Nabii huyo alisema, nalo Neno la Mungu lilikuwa pamoja na nabii, akasema, “Usiende huko juu. Na kama ukienda, Mungu hatakuwa pamoja nawe.” Huh! Lakini walidhani wangeenda haidhuru, “Mungu ni mwema sana, atafanya hivyo, mwajua, hatatufanyia lolote. Mungu yu pamoja nasi, kwa hiyo tunajali nini?”

170 Pentekoste, kamwe usiliingize hilo kichwani mwako. Wanawake: “Ninaweza kukata nywele zangu, naweza kufanya *hili*, naweza kufanya *lile*.”

Wanaume: “Ninaweza kufanya *hili*, ninaweza kwenda namna *hii*, mradi tu mimi ni wa . . .”

“Mungu aliniponya wakati mmoja.”

“Mungu alinipa Roho Mtakatifu wakati mmoja.”

“Mungu alifanya *hili*, Mungu alifanya *lile*.” Hiyo ni kweli, lakini usivuke mstari huo wa kutenganisha.

171 Musa alisema, “Mkienda huko juu, siendi pamoja nanyi. Nao Waamaleki na Wakanaani wako huko juu.” Nami nitawaambia ya kwamba dhambi imevuka mipaka ya Neno la Mungu, kutokuamini nukta moja Yake, Mungu atakuacha uketi hapo.

172 Loo, ni kazi kubwa *sana*, jambo baya sana! Ninawapenda watu, kwa nini inibidi kufanya hivi?

Jiunge, endelea tu kama hao wengine, “Mradi tu, mimi ni mfuasi wa kanisa, inaleta tofauti gani?” *Hakika* inaleta tofauti.

173 Maskini yule nabii aliwaambia Israeli jambo lile lile, akasema, “Je, niliwahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lilitimia?”

Wakasema, “La, yote uliyosema, Samweli, yote yalitimia.”

Kasema, “Je, niliwahi kwenda na kuchukua sadaka miongoni mwenu kujenga majengo makubwa, na kadhalika?”

“La, kamwe hukufanya hivyo, Samweli.”

“Vema,” kasema, “basi nisikilizeni, hamtaki kutenda kama mataifa mengine. Mungu ndiye Mfalme wenu.”

174 Nami ninasema leo hii, Pentekoste, msijaribu kutenda kama makanisa mengine, Mungu ndiye Baba yenu, Neno ndilo ngome yenu. Nimewahi kuwaambia lolote ila lilitimia? Nimewahi

kuchukua pesa zenu, na kuwasihi tuingilie miradi mikubwa, na mambo ya kila namna? Niambiени wakati mmoja nilipowahi kuchukua matoleo. Mnaona? Niambiени jambo moja lililopata kusemwa katika Jina la Bwana, ila lililotimia.

¹⁷⁵ Sasa, sikilizeni, dumuni na Neno, kwa kuwa Ujumbe wa siku za mwisho hauna budi, mjumbe na Ujumbe hawana budi kulingana na wakati wa mwisho, “Kuirudisha imani ya watoto kuelekea imani ya baba zao.”

¹⁷⁶ Hivi Yuda hakusema, kule, tayari wameninii... Kasema, “Mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu?” Miaka tisini na sita tu waliyokuwa nayo, ninaamini ilikuwa mwaka wa A.D. 96 tayari walikuwa wameiacha. Hivi hawakuingia na kuanza, likawa wa—wazo, halafu fundisho, ndipo basi likawa suala la Wanikolai?

¹⁷⁷ Neno *nikao* linamaanisha “kushinda,” “kumshinda huyo mama,” badala ya... “walei.” Badala ya vile ninyi nyote mmekuwa mkifanya hapa juu, kumwacha Roho Mtakatifu atende kazi miongoni mwa watu, kuna mtu mmoja mtakatifu. Ati mtu mtakatifu? Hakuna kitu kama hicho. Ni Roho Mtakatifu Kanisani. *Nikao*: “kuwashinda walei.” Ndipo—ndipo likawa fundisho.

¹⁷⁸ Jambo la kwanza walilofanya ni lipi? Wakaunda dhehebu. Mle ndani waliweka... Loo, na kwa mamia ya mamia ya miaka ilikuwa ni mateso kwa wote ambao hawangeinamia hayo, akavutwa vipande-vipande, na kuteketezwa, wakateswa. Ndipo moja kwa moja akaja Luther, huo Mti ukaanza kukua, na alipofanya hivyo akaunda madhehebu, Mungu akalikata hilo tawi, nalo likanyauka na kufa. Kama vile Yesu alivyosema, Yeye aliupogoa.

¹⁷⁹ Akaja yule Wesley, tawi lingine likitokea juu Yake. Walifanya nini? Wakaunda dhehebu. Mungu akalipogoa na kulikatilia mbali. Moja kwa moja ukaja Ujumbe wa tatu. Jinsi hasa Kanisa lilivyoanza, ule Mti wa Bibi-arusi hapo mwanzo, ukaanza. Ni nani aliyetangulia? Yohana, akihubiri kuhesabiwa haki, toba. Ni nani aliyefuata? Yesu Kristo, “Watakase, Baba, kwa ile Kweli, Neno Lako,” ambalo lilikuwa ni Yeye Mwenyewe, “ni Kweli,” utakaso. Ni kitu gani kilichofuata? Ubatizo wa Roho Mtakatifu, “Nawaletea juu yenu ahadi ya Baba Yangu,” ndipo Mti wa Bibi-arusi ukaanza kukua.

¹⁸⁰ Lakini huyu hapa parare anakuja, akaula *huu*; tunutu, akala tunda; wa pili, akala majani; huyo mwingine akala ganda; ndipo madumadu akaja, mnyonyaji, naye akaufyonza Uhai wenyewe kutoka kwake, na *kuwashinda* walei. Mungu akasema, “Nitaurudisha.”

¹⁸¹ Huu hapa ukaanza katika siku za Luther kisha ukaunda madhehebu. Mungu akaupogoa, kama alivyosema angefanya, Yohana 15. Akaja yule Wesley, vema, akaanzisha tawi zuri.

Walifanya nini? Wakaliundia dhehebu baada ya kifo cha Wesley. Wakaukatilia mbali. Wakaja Wapentekoste, wakileta hata ishara za tunda. Walifanya nini? Kuunda dhehebu. Umekatiliwa mbali. “Lakini nitarudisha, asema Bwana.” Atafanya hivyo.

¹⁸² Kuna shida gani na miamsho hii mikuu? Sasa, hebu na tuwe wenye busara. Tumekuwa na kile tumekiita “uamsho,” lakini tuliangua nini kutoka kwake? Wafuasi. Kwa nini? Kwa nini, enyi ndugu? Biblia ilisema katika Waebrania 6, “Mvua huinyeshea nchi mara nyingi, ili kuinyweshwa, kuitayarisha kwa ajili yake, tunda. Lakini miiba na michongoma iliyo karibu na kukataliwa itateketezwa.”

¹⁸³ Sasa, wana—wanayafunga matita yapate kuteketezwa, hiyo ni kweli. Yanafungwa matita, madhehebu haya yote, matita makubwa yanakuja kwenye tita moja kubwa. Hiyo ni kweli. Tita hilo ni nini? Mnajua ni kitu gani, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, likiunda sanamu ya mnyama, kweli.

¹⁸⁴ Nanyi watu mnaoogopa ukomunisti, nawatakeni mnionyeshe mahali pamoja katika Biblia ambapo ukomunisti utautawala ulimwengu. Vema, nitawaambia Biblia inasema ya kwamba Urumi utautawala ulimwengu. Kweli kabisa. Miguu inaenda wapi huko nje? Nabii yule, ambaye aliona ufalme wote wa Mataifa ukishuka moja kwa moja, mwishoni haukuingia katika ukomunisti, uliingia Urumi. Kweli kabisa.

¹⁸⁵ Sisi hapa katika siku hizi, watu wakidhania, wakijiunga moja kwa moja katika kitu hicho, kasema, “Hilo ni sawa, jambo ndilo hilo, hakika. Mimi ni mfuasi wa kanisa. Loo, naam, mimi ni *Nanii*.” Mnaona?

¹⁸⁶ Sasa, angalieni, Yeye alisema kutakuwako na Nuru wakati wa jioni. Hayo yataivisha jioni. . . matunda yanaweza tu kuiva kwa Nuru, tunajua hilo, na juu ya mti, Nuru ya jioni. Mengine yote. . . Lakini huko nyuma kabisa, hilo Neno la Mungu lililokusudiwa tangu zamani, lilikaa pale wakati wote kwa sababu Mungu alililena. “Nitalirudisha.”

¹⁸⁷ Atafanya hivyo, haidhuru ni madhehebu mangapi na kadhalika itambidi kupogoa, kutakuwako na Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi, “Kwa kuwa nitarudisha, asema Bwana.” Haina budi, kitu gani? Miaka yote iliyoliwa na parare, miaka yote iliyoliwa na madumadu, miaka yote ambayo madhehebu na wanyonyaji na kadhalika kwenye Mti huo waliyaondoa matunda Yake, wakaondoa matawi Yake, wakaondoa maganda Yake, wakautoa Uhai Wake, lakini, “Nitarudisha, kwa ajili ya Shina na Mzao wa Daudi. . . ? . . . nitarudisha, asema Bwana.”

¹⁸⁸ Ni kitu gani? Yeye alisema hivyo, Yeye alilichagua kimbele, Neno Lake liko hapa, kwa hiyo angalia, jinsi hasa alivyolifanya mara ya kwanza, Yeye alimchukua Yohana, kuhesabiwa haki; Yesu alilitakasa Kanisa kwa Damu Yake Mwenyewe, ndipo Roho

Mtakatifu akaja; ndipo baadaye Kanisa likaja, likaanza kukua, Luth- . . .

¹⁸⁹ Ndipo hapa wakaja hawa mchwa wanne, mmoja, mdudu yule yule, katika hatua mbalimbali tu, kisha akaja tu—tunutu. Alifanya nini? Jambo la kwanza, alikula tunda, upendano wa ndugu, kutoka kwake. Kitu kilichofuata kilikuwa ni parare, akaja, mdudu mwingine akaja, naye akala furaha, majani, ushirika. Mwingine akaja. Alifanya nini? Alikula maganda, parare. Ni yupi aliyefuata? Madumadu, naye akaunyonya Uhai moja kwa moja kutoka Kwake, lakini kulikuwako na Kisiki, maana Yoeli alisema, “Nitarudisha Shina hilo lililochaguliwa tangu zamani.” Haleluya!

¹⁹⁰ Nayo hayo majina yote ambayo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu yalikusudiwa, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Naam, bwana. “Wote aliotangulia kuwajua Yeye huwaita, wote anaowaita Yeye huwahesabia haki, na wale aliowahesabia haki, amewatukuza.”

¹⁹¹ Paulo, kulingana na Waefeso 1:5, au, Waefeso 1:5, Alisema, “Mungu alituchagua tangu zamani, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, tupate kufanywa wana wenye mamlaka katika Yesu Kristo.” Utalikomeshaje? Pepo wote kuzimuni, afadhali muache kulizozania, litakuwepo bila waa wala kunyanzi. Litakuwa Nini? Kanisa la Bibi-arusi. Haleluya! Mungu alisema, “Nitarudisha.” Kurudisha Nini? Moja lisilo na mguso wa madhehebu, Moja lililo na Neno safi lisiloghoshiwa; halina budi kuja.

¹⁹² Kwa nini tulipata kundi la madhehebu, wakati huu, kutoka kwenye uamsho huu? Tulipanda mbegu ya kimadhehebu. Kile tunachohitaji leo hii, ndugu, unaweza kusema unachotaka kukihusu, tunahitaji kupandwa kwa Injili, Neno safi, takatifu, lisiloghoshiwa la Mungu, ambapo wakati Nuru hii itakapotokea, italileta Kanisa hilo, lililochaguliwa na Mungu tangu zamani. Amina. Usidhanie chochote, chukua Neno la Mungu na uendelee moja kwa moja. Aliahidi angekuwa hapa, Yeye yupo hapa. Amina. Afadhali nisimame.

¹⁹³ Imezidi sana, “Mungu mwema. Ananipenda kupita kiasi hata hawezi kuniadhibu.” Aliahidi jambo hilo. Alimpenda Adamu, alimpenda Hawa, Yeye ni Upendo, bali Yeye ni mwenye haki, hana budi kulitimiza Neno Lake. Kama unaamini *Hili* kuwa ni Neno la Mungu, chochote kinyume na *Hili*, “Mtu yeyote atakayeondoa, ama kuongeza kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake ya Kitabu cha Uzima,” mhubiri, ama dhehebu, ama chochote kile.

¹⁹⁴ Vipi kuhusu kanuni hizi zote za imani na kadhalika zilizoundwa miongoni mwa wanadamu? Mungu kamwe hashughuliki na kundi, Yeye hushughulika na mtu binafsi. Vikundi vina mawazo tofauti. Nionyeshe wakati mmoja

alipowahi kufanya hivyo; Yeye hushughulika na mtu binafsi. Anashughulika na wewe, anashughulika na mimi, anashughulika na mtu huyo mwingine. Hiyo ni kweli. Ni jambo la mtu binafsi.

¹⁹⁵ Israeli walidhania ya kwamba Yeye alikuwa mwema sana, walikuwa wameona mambo mengi sana hata wangeweza tu kufanya lolote walilotaka, kama yule mvulana tineja. Hivyo ndivyo kanisa lilivyo siku hizi, wanavyojisikia, “Vema, Mungu alinipa Roho Mtakatifu, kama nikitaka kufanya *hili* ninaweza kufanya. Haleluya! Hakuna hukumu ndani yangu, niko ndani ya Kristo.” Hilo, papo hapo, linaonyesha ya kwamba huko humo. Kama ndivyo, ulikuwa ndani ya Kristo, ungeshikilia Neno Lake haidhuru mtu yeyote alisema nini, kama ilikubidi kusimama peke yako ungeitetea, maana ni Roho wa Mungu ndani yako akilithibitisha Neno Lake.

¹⁹⁶ Hakuna hata Neno moja Lake litakalopita mpaka limetimizwa, ni la thamani sana, na la kupendeza sana. Ni kama tu vile, Mungu, Yeye halihukumu kwa kanisa, Yeye hauhukumu ulimwengu kwa madhehebu, Yeye hulikumu Kanisa kwa ninii Yake, ama, huuhukumu ulimwengu kwa Neno Lake, kama alivyowafanya Hawa na Adamu. Jinsi Mungu anavyoanza, hawezi kumalizia vinginevyo, hana budi kumalizia vile vile alivyoanza, kama hakufanya hivyo, alikosea kwa kuanzia. Mnaona?

¹⁹⁷ Usidhanie, amini. Usithubutu bila mamlaka, bila mamlaka ya Kimaandiko. Samsoni alidhania, “Loo, vema, jamani! Loo, najua ninaninii... siwezi... Sina vishungi vyangu tena, lakini nadhani ni sawa, ningali ni maskini jamaa yule yule.”

¹⁹⁸ La, la, Ndugu, umevuka mstari wa utengano. Alidhani alikuwa tu na nguvu nyingi kadiri alivyoweza... Kasema, “Nitajinyosha tu. Loo, whiu! Sasa, mimi ni mtu mzuri tu kama nilivyowahi kuwa.” Lakini alikuta kwamba nguvu zake zilikuwa zimemwisha.

¹⁹⁹ Hivyo ndivyo tulivyofanya wakati huu uamsho ulipoanza yapata miaka kumi na minne iliyopita, Mpentekoste aligundua kwamba asingeweza kujinyosha tena, kwa sababu alikuwa amejiundia madhehebu katika makundi madogo-madogo, nao walichukiana, wakapanda hayo mafarakano miongoni mwa ndugu, ndipo uamsho ukashuka, nayo Nuru ya jioni ikaingia, lakini yeye alifanya nini? Asingeweza kufanya lolote, kwa sababu amejiundia madhehebu. Amepoteza nguvu zake, upendano wake wa kindugu, matunda ya Roho.

²⁰⁰ Samsoni aliwazia, “Yeye angali yumo humo. Siwezi...” Afadhali uwe unahisi. “Angali yumo humo.”

Akani aliwazia, alipochukua ile kabari, “Loo, haitaonekana.”

201 Loo, mhubiri yule pale aliniambia, “Loo, Ndugu Branham, je, inaleta tofauti yoyote kama ni *hivi*, ama *vile*?” Hakika inaleta tofauti. Huo ndio uongo wenyewe ambao Shetani alimwambia Hawa. Inaleta tofauti.

202 “Vema, mradi tu hao wengine wanafanya hivyo!”

Sijali ni nani anayelifanya, ama ni nani asiyelifanya.

“Ninataka kulifanya, kwa vyovyote vile!”

203 Sidhanii ya kwamba hilo ni sawa kwa sababu hao wengine hufanya hivyo, Mungu anahitaji *hili*, na *hili* ndilo sina budi kuwa nalo. Hao wengine wasipokuja, ninaweza tu kulisema, niendeleo tu kusonga mbele, bila kudhania chochote juu Yake.

204 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . nahitaji watu zaidi leo kama Mikaya, wanaoweza kusimama na kusema yale hasa Mungu aliyosema, wasiopunguza nguvu za mashambulizi popote. Amina. Naam.

205 Udhaifu, Akani alisema, “Haitaonekana, haileti tofauti yoyote.” Bali ilileta tofauti, kabari hiyo moja ndogo ilivuruga mpango wote wa Mungu.

206 “Batizwa tu kwa njia yoyote, haileti tofauti yoyote. Ninii tu, maadamu wewe ni mfuasi wa kanisa, haidhuru.” Hilo ndilo lililouvuruga uamsho, hiyo ndiyo shida, tuna kundi la madhehebu. Badala ya kuwa na watakatifu, tuna wenye kujiunga, watoa maamuzi.

207 Jiwe linafaa nini bila mwashi wa kulikata, na kulichonga, na kuvunja pembe zake? Unapomwona mchongaji amesimama, akifanya kazi juu ya jiwe, haionekani kama ni kitu, bali niani mwake anajua anachotaribu kufanya. Kwa hiyo alibingirisha jiwe kule juu kwa kusudi fulani naye hana budi kulichonga, na kulikata, na kulinoa.

208 Mawe yanayokiri kuwa ni Wakristo ambayo yatatoka hapa nje na kutenda vyovyote, na kudhania *hili* ni sawa, kudhani *lile* ni sawa! Wanasimama kimya, naye Mchongaji, Roho Mtakatifu, anawakata wakawa sura za wana na binti za Mungu. Loo, utukufu! Yeye ni Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni, Nyota ya Asubuhi, Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho, Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja, Shina na Mzao wa Daudi. Haleluya! Naam.

209 Kudhania ni sawa, Wamisri, waliwaona Israeli, waliotahiriwa, wakivuka Bahari ya Chumvi, walidhani kwamba walikuwa ni watu wazuri tu kama walivyokuwa. Walienda nyuma yao na kuzama ndani yake, walidhani ilikuwa ni sawa. Sina budi kuharakisha.

210 Wakati wa Nuhu, walidhani kama ikija gharika kama Nuhu alivyosema ingekuja, vema, jambo pekee wangepanya, ni kurukia mashua yao wenyewe. Lakini kulikuwa na mashua moja pekee iliyotengenezwa na Mungu.

211 Hivyo ndivyo ilivyo na watu siku hizi, wanasema, “Mimi ni mfuasi wa kanisa. Ninafanya *hili*, nafanya *lile*.” Lakini basi kuna Kundi moja tu lililoundwa na Mungu, na hilo halijaundwa kimadhehebu, Limeundwa kwa Neno, katika ufunuo wa nguvu Zake, mashua iliyoundwa na Mungu. Usidhanie, amini tu Neno la Mungu.

212 Nuhu aliunda mashua hiyo kwa mti wa aina *fulani*, laiti tungalikuwa na wakati wa kuliingilia, bali hatuna, jinsi alivyochukua huo mti wa mshita. Uliwahi kuona? Ni mwepesi kuliko balsa. Mbona, kama mtu yeyote angemwona mtu akijaribu kujenga mashua kwa mbao za aina hiyo, wangesema ana kichaa. Kwa nini? Ndio mbao nyepesi kuliko zote. Ukitupa, ukitupa tu mbao za mshita huko nje majini, ni, zinafanya *swish*, *whiu*, zinazama papo hapo. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo, Yeye ananinii tu—anawapumbaza tu kwalo, wanaketi hapo, na wajinga kama sungura wakubwa. Akaketi pale . . . Akasema . . .

213 Lakini wangependa nini? Hawajaribu kuwa na hekima yao wenyewe, hawawezi kulelewa. Hupaswi kuliwazia, unapaswa kuliadini.

214 Kasema, “Chukua mbao za mshita.” Ni—ni—ni mwepesi tu, kama sifongo. Lakini sasa, angalia, baada ya kuiharibu miti hiyo yote ya mshita, kuijenga, hasa, Yeye alisema, “Enendeni mkachukue lami, mkailoweshe.” Loo! Walipataje lami katika siku hizo? Walichukua mti wa aina nyingine, msonobari, nao wakauponda-ponda, na kuuponda mpaka lami ikatoka ndani yake.

215 Ni mfano wa nini? Mbao alizo nazo Mungu siku hizi: Ondoeni upuuzi wenu wote wa kale wa ulokole, ondosheni madhehebu yenu yote, ichukueni nuru halisi na mkae tu mbele za Mungu. Ndipo akampiga Mmoja wetu, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu.” Alipigwa, na kujeruhiwa, na kuchubuliwa pale Kalvari, kusudi Roho Wake apate kumiminiwa ndani yako unapokuwa mtupu.

216 Halafu basi, mtumbwi huo, safina hiyo, wakati hiyo ilipowekwa mle ndani, hata msumari usingeweza kupigiliwa ndani yake, hiyo ndiyo sababu yale magogo makubwa yaliyoigonga yasingetoboa shimo ndani yake. Mbona, mwaloni, msonobari, wala chochote kingine, hakingeshikilia namna hiyo. Mnaona, ulikuwa tayari umelowa maji, ukapakwa lami ndani na nje. Hiyo ni kweli.

217 Hivyo ndivyo Mkristo alivyo, yeye hujifanya tupu, “Sitaki kujua kile mtu yeyote . . . Ninataka kujua, Bwana, nataka kukujua Wewe; ninakutaka Wewe, mapenzi Yako, Uzima Wako.” Ndipo Mungu ananinii tu . . . wewe jizamishe tu ndani ya Kristo.

218 Vema, basi ilikuwa ni nini? Kwa kweli haungekuwa mti wa mshita tena, ungekuwa ni msonobari. Si wewe tena, ni Roho ndani yako. Unaona? Loo, jamani, iliyoundwa na

Mungu. Manabii wengi sana siku hizi, wakisema mambo mengi mbalimbali, huwafanya watu kuchanganyikiwa. Usidhanie, angalia tu ahadi Yake iliyothibitishwa.

²¹⁹ Hebu tuone, Kumbukumbu la Torati 18:22, Mungu alisema, “Akiwepo mtu miongoni mwenu aliye wa kiroho au nabii, na yale asemayo yanatimia, basi msikieni, yasipotimia, basi msimsikie.” Yohana 14:12, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Marko 16 ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao, aminini,” si “watajiunga na kanisa, na kuandika jina lao kwenye kitabu, na kuishi maisha mazuri,” lakini, “katika Jina Langu watatoa pepo, na kunena kwa lugha mpya.” La, bwana.

²²⁰ Yohana kamwe hakudhania ya kwamba angeenda huko nje. Yohana, mwajua, wakati yeye. . . Alikuwa ametoka kwenye ukoo wa kuhani. Si ni ajabu? Yohana, ilionekana kana kwamba, kweli angefuata utaratibu wa baba yake, kwa sababu alikuwa ametoka kwa ukuhani mkali. Lakini mnajua, hiyo kazi ilikuwa kubwa mno, Yohana hakutaka kujichanganyisha na yoyote ya theolojia yao.

²²¹ Mungu alimpeleka huko nyikani, peke yake, na kumfundisha huko nje, kwa kuwa Yeye alisema, “Yohana, watakuwa na mambo ya kila namna, na kukufanya uamini kila namna ya mambo yasiyo ya kimaandiko, bali litakuwa hili hapa, Yohana: Yule ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu Yake, Huyo Ndiye atakayebatiza.”

²²² Haikumbidi Yohana kusema, “Nadhani kwamba *huyu* ni mtu mzuri. Nadhani kwamba *huyo* ni mtu mzuri. Nadhani atakuja kwenu Mafarisayo, ninyi wa Umoja, ninyi wa Utatu, ninyi *hili*, hao ndio Yeye atakaowajia.” Yohana alisema, “Yule ambaye nitamwona Roho akimshukia!” Utukufu!

²²³ Ndugu, si dhehebu lako. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Haikubidi kuwa na wasiwasi, kushangaa, Mungu tayari amesema la kutazamia, matunda ya jioni, Nuru ya jioni.

²²⁴ Alisema katika siku za mwisho itakuwa, ibilisi angewatuma wahudumu wake, malaika wa nuru, wakijaribu kuwaleta kitu kipya, kitu maarufu zaidi, kitu chenye elimu zaidi, msiamini hilo, hivyo ndivyo Hawa alivyofanya ndipo akaingia katika shida, dumuni na Neno. Amina. Usidhanie, lichukue Neno la Mungu. Hawa alidhani ilikuwa ni sawa, “Mungu ni Mungu mwema. Unajua asingeweza, *hakika*, Bwana hatafanya *hili*, wala kufanya *lile*.” Lakini Mungu alikuwa ameahidi jambo hilo, ilimbidi Mungu kulifanya, ilikuwa ni wajibu wa Mungu kulifanya. Sasa, usidhanie, amini tu.

²²⁵ Yohana alisema, “Nilimjua, maana niliona ishara ya Masihi juu Yake, nami ninajua huyu Ndiye.” Hakudhania.

226 Haikumbidi Nathanaeli kudhania, hata kidogo, wakati Yeye alipomwambia, alijua—alijua yale Kumbukumbu la Torati 18:22 iliyosema, kwa hiyo wakati aliposema, “Wewe ni Mwisraeli kwelikweli, huna hila”:

Alisema, “Ulinijua lini Wewe? Ulipata kuniona lini Wewe?”

Akasema, “Kabla Filipino hajakuita.” Haikumbidi kudhania.

227 Akasema, “Rabi,” Hmm! “Rabi, Mwalimu, ingawa shule zinayadhihaki Mafundisho Yako, wanakukataa kwa sababu ya Mafundisho Yako, lakini Rabi, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.” Hakudhania, alikuwa na ushahidi wa Kimaandiko wa jambo hilo, hivyo ndivyo Masihi angefanya, hakudhania.

228 Maskini huyo kahaba mchafu, anayevunda, labda madhehebu yote nchini labda yalikuwa yamemtenga, lakini kwanza kabisa yeye hakuona chochote ndani yao. Wakati angeona Kitu fulani halisi, angekichukua. Kwa hiyo akamwona Myahudi wa kawaida ameketi pale, akawazia, alionekana kama mtu wa kawaida, hakuwa na ukosi uliopinduliwa, kilemba kikubwa mno, Dk. Kasisi Baba Mtakatifu, alikuwa ni Mwanadamu tu, aliyevalia kama watu wengine. Ameketi, akainama huko nyuma, labda ana mvi kidogo, alikuwa tu na umri wa miaka thelathini na kitu, bali Biblia ilisema, mwajua, alionekana mwenye umri wa miaka hamsini. Mlijua hilo?

Walisema, “Unasema . . . Wewe si mtu mwenye umri wa zaidi ya miaka hamsini, nawe unasema umemwona Ibrahimu? Sasa tunajua ya kwamba wewe ni, una pepo.”

Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Hmm! Unaona?

“Sasa tunajua una pepo.” Mnaona, wao ni vipofu.

Akasema, “Enyi Mafarisayo vipofu, vipofu wakiwaongoza vipofu.” Mnaona? Jambo ndilo hilo.

229 Sasa, tunamwona ameketi pale, maskini mwanamke huyo akamwambia, akasema, “Vema, mnataka, ninyi Wayahudi, mnataka kubishania dini.” Hiyo ilikuwa ndiyo desturi ya siku hiyo, kama ilivyo siku hizi. “Ninyi Wayahudi mkisema ni *hapa*, na *hapa chini*, na wote *hiki-na-hiki*, nasi tunasema . . .”

Akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

Kasema, “Hiyo ni kweli. Unao watano; na yule unayeishi naye sasa siye wako.”

230 Angalieni, upesi, hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani imekaa pale! Utukufu! Jamani! Kitu gani? Isingekuwa kitu kingine chochote, hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani. Basi wakati Maji hayo yalipoanza kuishukia Mbegu hiyo, ilianza kuchanua. Haikukubidi kumwambia, alijua. Akasema,

“Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Tunajua Masihi yuaja, tunamtazamia, na ajapo, Yeye atatuambia mambo ya namna hii.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

Akasema, “Hilo ni zuri vya kutosha kwangu.” Hakuna kudhania.

²³¹ Hakuingia, aseme, “Aisee, ninyi Madaktari wa Uungu, ningetaka kuwaingiza nyote katika hoja ya Kimaandiko.” Akasema, “Sidhanii chochote. Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Kristo?” Jambo ndilo hilo. Haikumbidi kudhania, kuthubutu bila mamlaka, alikuwa na mamlaka, alikuwa na mamlaka ya Kimaandiko kuamini jambo hilo.

“Loo, ewe mwanamke, hujui, wewe si wa shule yetu, wewe si mfuasi wa lolote la madhehebu haya.”

²³² Kasema, “Sijali usemalo, ninajua BWANA ASEMA HIVI ni nini. Walisema atakuwa ni Nabii, naye Huyu *hapo*.” Amina. Alikuwa na mamlaka ya Kimaandiko, hakudhania.

“Hili lilitoka kwenye shule gani?”

“Lilitoka kwenye Biblia.” Hiyo ni kweli. Loo, hakika.

²³³ Wale wanafunzi kwenye Pentekoste: Sasa, ninyi Wapentekoste, vaeni kofia zenu, mnaweza kupaza sauti kwa hili, mnaona. Angalieni, vipi kama hao wanafunzi wangesema, “Vema, sasa, sikilizeni, nawaambia . . .”

²³⁴ Mathayo anaenda pale, na kumwambia Petro, “Petro, nataka kukuuliza jambo fulani. Hivi Bwana wetu hakutuambia tungoje hapa juu, tuje huku, Naye alikuwa anaenda kututumia Ahadi ya Baba juu yetu?”

“Loo, hakika. Naam,” Petro akasema, “hiyo ni kweli. Unaonaje, Marko?”

Marko, “Loo, hakika, Yeye alisema hivyo. Naam. Alisema atafanya hivyo.”

²³⁵ “Vema, ndugu, tumekuwa hapa siku tisa. Mwajua, hivi majuzi nilikuwa na hisia ya ajabu. Mwajua, kwa namna fulani ninaamini tu jambo hilo, hivi hamdhanii ya kwamba hatupaswi kungojea zaidi? Nadhani tayari tumempokea, maana Yeye alitwambia tungoje hapa. Vema, hapa, ninaamini, tayari tumekuwa hapa siku tisa, kwa hiyo nadhani afadhali tuendelee na huduma yetu. Nadhani tayari tumempokea, kwa sababu tulimtii.”

²³⁶ Hapo ndipo ninyi Wapentekoste mlipomkosa kwa maili milioni moja, mlifuata mhemko, badala ya kungojea Neno litimie. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu mliunda dhehebu. Hiyo ndiyo sababu mliwasikiliza hao. . . Sikuzote viongozi ndio wanaowatoa watu nje ya mapenzi ya Mungu.

²³⁷ Ilikuwa ni Kora. Si...Ilikuwa ni Kora, yule kiongozi asiyevuviwa, ambaye alisema, “Wao...Musa anajaribu kufikiri yeye ndiye mtu mtakatifu pekee. Mbona, tunao watu watakatifu kiasi hicho hapa, tuna makundi hapa nje! Hivi Mungu hakuweka roho ya unabii juu ya watu *hawa* wote? Akaitoa kwa Musa na kuiweka hapa. Kwa hiyo tutasikiliza tu kundi *hili*. Musa anafikiri yeye ni *kitu*.”

²³⁸ Mungu akamwambia Musa, “Jitenge naye, nita—nitamzamisha yeye pamoja na kundi lake, dhehebu lake lote.” Kweli. Musa alikuwa kiongozi wa Mungu. Musa alithibitishwa kuwa ndiye kiongozi huyo, wote wasiomsikiliza waliangamia. Yesu alikuwa Kiongozi wa Mungu. Roho Mtakatifu ni Kiongozi Wake, na wote wasiomtii Roho Mtakatifu, aliyeiandika Biblia hii, wataangamia. Amina.

²³⁹ Kasema, “Ngoja. Tungojeni tu.”

“Ninaamini, nawaambia sasa, tumempokea. Hebu tutoke tu nje.”

²⁴⁰ La, hawakufanya hivyo. Walijua ya kwamba Isaya 28:11 ilisema, “Amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo, na pale kidogo. Shikilia sana yaliyo mema. Kwa kuwa kwa midomo ya wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa. Na huku ndiko kuadhimisha sabato, raha inayomfanya yeye aliyechoka...” Walijua ya kwamba Maandiko hayana budi kutumiwa zaidi tena, ama muda gani waliongojea, ama yale waliyofanya. Hawakuwa wakidhania chochote, walikuwa wakingojea Maandiko yatimie.

²⁴¹ Walijua ya kwamba Yoeli alisema... Msikilize Petro akiruka moja kwa moja huko nje, katika dakika chache baadaye... ndipo kesho yake akahubiri juu ya Yoeli. Yoeli alisema, “Na itakuwa,” Yoeli 2:28, “katika siku za mwisho kwamba nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; wana wenu na binti zenu watatabiri. Na juu ya watumishi Wangu waume na wanawake nitaimwaga Roho Yangu. Nitatoa ishara katika mbingu juu, na maajabu katika nchi chini, moto na nguzo za moshi, na mvuke. Itakuwa kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya. Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.”

²⁴² Walikuwa wakingojea, hawakuwa wakidhania walikuwa na chochote, walikuwa wakingojea mpaka Maandiko yalipodhihirishwa. Utukufu! Loo, ndugu, laiti isingekuwa imechelewa hivi. Jinsi tungetaka kukaa hapo kwa muda kidogo! Walingojea mamlaka ya Kimaandiko.

²⁴³ Siku hizi, tunachukua tu kanuni ya imani, mhemko, moshi kidogo, ama moto, ama mhemko mdogo, mtu fulani aseme, “Utukufu kwa Mungu, tumempokea. Haleluya! Mnaona mafuta mkononi mwangu? Angalieni *hapa* juu.” Loo, jamani! Angalia kichwa chako, kiko katika umbo la namna gani. Unaona? Sikusema hivyo nipate kuwa mwerevu, kunradhini,

nisameheni. Sikulimaanisha, sikupaswa kusema hivyo. Kitu fulani kiliniambia tu, “Usiliseme.” Achana nalo, “Kipofu akimwongoza kipofu, wataanguka shimoni.” Vema.

²⁴⁴ Bila mamlaka ya Kimaandiko, wanalichukua kwa kanuni ya imani, “Ikariri kanuni *hii* ya imani.” Wanadhani hilo ni sawa. Wanaendelea, wanalichukua kwa mhemuko, “Loo, utukufu kwa Mungu, nilinena kwa lugha usiku kucha.” Nimeona pepo wakifanya jambo lile lile. Mnaona? Hakika.

²⁴⁵ “Huamini, basi, katika kunena kwa lugha?” Hakika, ninaamini; hilo silo. Mimi ni mmishenari, nimewaona wakinywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kunena kwa lugha, na kumwita ibilisi. Bila shaka, loo, naam. Mama yangu, ndio kwanza tumzike hivi majuzi, alikuwa nusu Mhindi, nimekuwa kwenye kambi, na nikamwalia mchawi akinena kwa lugha, na kuweka penseli chini, inainuka na kuandika katika lugha zisizojulikana. Bila shaka. Usiniambie hilo ndilo. Loo, la, la. Rehema, jamani!

²⁴⁶ Baadhi ya watu wanaonena kwa lugha wanadai wana Roho Mtakatifu, na kukana nusu ya Neno Lake, na wakati mwingine nguvu Zake zote. Roho Mtakatifu atalishuhudia Neno Lake. Roho Mtakatifu anawezaje kukwambia ufanye jambo fulani, kisha ageuke, aseme, “La, ni sawa, endelea tu na ufanye hili *lingine*.” Hatafanya hivyo. Hakulifanya hivyo, na Hawa, hakulifanya hapo mwanzo. Kama akilifanya sasa wala hakulifanya pale, basi Yeye si mwenye haki, Yeye alisababisha mateso haya yote, wakati tungalikuwa hapa kwa vyovyote vile.

²⁴⁷ Mungu ni Mkandarasi mkuu, miili yetu iliwekwa hapa nje, lakini, wakati ulimwengu ulipojengwa, sisi ni kalisi, potashi, petroli, nurulimwengu, elementi kumi na sita mbalimbali za ulimwengu ziko ndani yetu, naye Mungu aliumba ulimwengu kabla hajamwamba mwanadamu, Yeye ni Mkandarasi, aliuweka, alikuwa awaite kutoka katika mavumbi ya nchi, lakini Hawa hakuliamini Neno la Mungu, yodi moja ndogo, na ikawafanya wanawake wawazae watoto.

²⁴⁸ Lakini Neno hilo la Mungu lililokusudiwa tangu zamani lililowekwa huko litamleta huyo aliyechaguliwa tangu zamani, wakati Yeye atakaponena, atatoka duniani katika ufufuo. Haleluya! Si ajabu Ayubu: “Najua Mkombozi wangu yu hai, siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu wa ngozi watauharibu mwili huu, Yeye atanena nami nitajibu, Yeye ataita, nami nitamjibu.” Hakika. Amina. Hmm! Nikomee wapi?

²⁴⁹ Ukisema una Roho Mtakatifu, na ulinena kwa lugha na kukuuliza, “Je, umempokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini? Vema, basi, ulibatizwaje?”

“Haileti tofauti yoyote.”

“Inaleta.”

“Vema, mimi hufanya *hili*. Haileti tofauti yoyote kama nikivalia *hivi* ama *vile*.”

“Biblia inasema inaleta.”

“Haileti tofauti yoyote kama nikifanya *hivi*, ama *vile*.”

“Biblia inasema inaleta.” Haya basi. Afadhali uachane nalo, acha waalimu waseme hilo basi. Vema.

²⁵⁰ Leo hii tunalichukulia kijuu juu, tukidhania, tunasema tunalo, “Naam, hakika, nilifanya *hili*. Ni—nilitetemeka usiku kucha. Mnajua nini? Nina damu mikononi mwangu, hiyo inaonyesha ninayo.”

²⁵¹ Ati una damu mkononi mwako? Huenda ukawa na hiyo, kisha ugeuke, na kulikana Neno la Mungu. Na kusema ati una Roho Mtakatifu? Roho Mtakatifu atasema, “Amina,” kwa kila Neno, maana Yeye aliliandika Neno, Yeye ni Neno. Hakika. Acha kudhania, ngoja mpaka hasira hiyo yote, dhambi, na mambo ambayo yamekuondokea, kusudi Mungu aweze kukujaza.

²⁵² Musa, wakati mmoja alidhani, kwa sababu, bila shahidi, ama, bila ujuzi, alikuwa amesikia Neno ya kwamba angekuwa mkombozi, bali hakuwa na wito, hakuwa na ujuzi, kwa hiyo akadhani ya kwamba angeweza kutoka moja kwa moja na kuchukua mamlaka.

²⁵³ Hivyo ndivyo watu wanavyowazia siku hizi, “Loo, tutakuwa na uamsho, tunataka kuona uamsho katika wakati wetu. Nyote fanyeni maungamo yenu, tunataka—tunataka mawe zaidi. Tunataka *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Tu—tunataka maamuzi yafanywe.”

²⁵⁴ Ni kitu gani? Utakuwaje na uamsho juu ya hilo, wakati unapopanda mbegu za Kibaptisti, Kimethodisti, Kipentekoste, na Kipresbiteri, na kukana Mbegu ya Mungu, Neno? Yesu alisema Neno ni Mbegu, Biblia; Neno la Mungu ni Mbegu. Utaletaje Kanisa la Biblia kwa mbegu ya kimadhehebu?

²⁵⁵ Vema, unasema, “Mungu asifiwe, Ndugu Branham, Roho Mtakatifu alifanya *hili*, nilipaza sauti na kupiga mayowe.” Hivi ulijua maji yale yale yaliyotumwa kukuza ngano, hu—hufana gugu linalovunda kufurahi tu kama yanavyoifanya hiyo ngano? Liliingiaje mle? Hufanya mtambaaji, hufanya miiba. Kwa nini? Yanaona kiu, yako kondeni wakati ninii. . . “Mvua huwanyea wenye haki na wasio haki.”

²⁵⁶ Kasema, “Nilipaza sauti, Ndugu Branham. Nilicheza katika Roho. Nilinena kwa lugha.” Ninaamini katika mambo hayo pia. Lakini linazaa tunda la aina gani? “Kwa matunda yao mtawatambua.” Tunda la Roho ni Neno la Mungu likijidhihirisha Lenyewe: upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, saburi, imani. Imani katika Nini? Neno. “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.” Haina budi kufanya hivyo. Hakika.

257 Musa alidhania, “Loo, nina maarifa tele, nitafanya hivyo.” Lakini hakuwa na wito, hakuwa na ujuzi. Hakika. Alitoka nje akidhania, akidhania kuhusu jambo asilopaswa kufanya. Lakini baada ya kukutana na kichaka kilichowaka moto kule juu siku moja, loo, ndugu, alipoisikia Sauti ya Mungu!

258 Alimpa msingi wa Kimaandiko, si yale mama yake aliyomwambia, bali yale Mungu aliyomwambia, “MIMI NDIMI Mungu wa Ibrahimu, MIMI NDIMI Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo,” akamwita jina lake la kifalme, akampa jina lingine. “Nimesikia kilio cha watu Wangu, nimeona mateso yao kwa mnyapara. Ninalikumbuka Neno Langu lililoahidiwa.” Haleluya! Haya basi. Utukufu!

259 Angali anakumbuka Neno Lake lililoahidiwa, “Nitarudisha, asema Bwana, yote ambayo wadudu wa kimadhehebu, na nyenje, na tunutu, na parare, na madumadu wamekula, *itikadi* zao zote za kimadhehebu na kanuni za imani na kadhalika ambazo wamekula. Ninalikumbuka Neno Langu, nami nimeshuka chini miongoni mwa watu. Nitarudisha, asema Bwana.”

260 Usidhanie ni kweli, Biblia inakwambia yaliyo mema na mabaya. Whiu! Afadhali tuache, nimewaweka saa moja zaidi. “Nitarudisha.” Usidhanie. Roho Mtakatifu yupo hapa, Biblia iko hapa, Roho Mtakatifu hushuhudia Neno la Mungu, kila ahadi na nukta, anasema, “Amina,” kwake.

261 Usidhanie ni sawa kwa sababu ulikuwa na mhemko. Tujichunguze asubuhi ya leo, tuangalie kote na tuone kile tunachoamini. Tuone kama sisi, kama Mungu alisema Jambo *fulani*, kama tungekubaliana Nalo. “Vema,” unasema, “Nitafukuzwa kanisani mwangu kama nikifanya *hivi* ama nikifanya *vile*.” Vema, ni lipi la zaidi kwako? Mungu wako au kanisa lako? Usidhanie bila ujuzi.

262 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Ndugu Branham, hivi huamini katika toharani?”

Nikasema, “Hakika.”

“Loo, naona wewe ni Mkatoliki.”

Nikasema, “Naam.” *Katoliki* maana yake ni “la ulimwenguni kote.” Mimi ni Mpentekoste-Mkatoliki mkuu wa lile Kanisa la asili.

263 Mtu fulani alisema wana tangazo sasa, Papa Yohana wa XXII, ama, ishirini- . . . , LII, ama kitu *fulani kingine*, alisema— alisema, “Watu wote wanarudi kwenye Kanisa la asili. Kanisa la asili lilianza Rumi.”

264 Huo ni uongo. Utukufu! Kanisa kamwe halikuanzia Rumi. Nitakubaliana na huyo mtu: Kanisa na lirudi mahali lilipoanzia, Pentekoste. Utukufu! Rudi mahali ulipoanzia, hapo ni ninii ya Mungu . . . ? . . . kwa kuwa Yeye atalirudisha.

265 Hakika, madhehebu yanarudi Rumi yalikutoka, lakini, haleluya, Mungu atairudisha Pentekoste, iirudie imani ya—ya baba zao. Haleluya!

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa. (Kila
doa la kutokuamini.)

266 “Tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho.” Roho Mtakatifu, kupitia kwa mtu ambaye asingekudhuru kwa chochote. . .Ningewezaje kuwadhuru watoto wa Mungu? Lakini jisalimishe na uone Neno likitokea, Hilo ni Mtahiri, linakata kufikia moyoni, linajua yale hasa unayowazia, na kuyaleta tena moja kwa moja kupitia kwenye vyombo vile vile. Amina.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wasioamini;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

267 Hivi hamuupendi huo? Mnafikiri ninawapenda? Hakika ninawapenda. Ninyi ni urithi wa Mungu. Mara nyingi nimewazia, “Ningefanya nini kama ningekuwa na matone mawili ya Damu halisi ya Yesu katika bilauri, nikiyashikilia, ile Damu iliyodondoka kutoka kwenye, mishipa Yake, kutoka msalabani, nami nilikuwa nayo. Jinsi ningeshikilia moyoni mwangu, na kutembea, kuangalia kila hatua. . .? . . . nikiithamini hiyo Damu, matone mawili tu ya Damu halisi, jinsi ningeshikilia!”

268 Lakini mnajua nini? Kulingana na Mungu, nimeshika chini yangu asubuhi ya—ya leo, machoni Pake, kilicho kikuu kuliko hiyo: ninacho kile kilichonunuliwa kwa Damu Yake. Hiyo ndiyo sababu ya kumwaga Damu Yake, kuwanunua. Ninapaswa kuwashughulikiaje? Je, ninaweza kuona dhambi ikianza kunyemelea ndani na—na kuwachafua? Loo, la, la, siwezi kufanya hivyo, sina budi kuvisukumia mbali vitu hivyo, nivikatilie mbali. *Hili* Ndilo, dumu na Neno, ndugu. Mnampenda?

269 Asanteni kwa kukaa pamoja nami, mkisaidia. Ni saa sita na dakika thelathini, nami nasikitika nilininii. . .La, sivyo. Mungu anisamehe, ni kosa kusema hivyo. Sikuhusika nalo, Yeye alilifanya Mwenyewe. Tena na—tena na—nawapenda tu, ninawaamini.

270 Ninaamini ya kwamba Mungu atakuwa na Kanisa, nami ninaamini ninyi ni sehemu ya Kanisa hilo. Tena ninawapenda kwa upendo wa kiungu. Pia naomba ya kwamba Roho

Mtakatifu ataruhusu Neno hilo lifasiriwe katika Roho ambayo lilikusudiwa, wakati likiwajieni.

²⁷¹ Sasa, ninampa mchungaji we—wenu. Sasa, kama mnaweza, rudini usiku wa leo, na muwe pamoja nasi tena, usiku wa leo. Iweni kwenye ubatizo alasiri ya leo huko nyumbani kwa Ndugu.

²⁷² Njoo hapa, Ndugu Parker. Samahani kwa kuliita jina lako la kwanza, lakini walisema, “Petro, Yakobo, Yohana,” kadhalika.

Mungu akubariki, Ndugu Parker. 🕊

62-0610M Kudhania
Aberdeen High School
Aberdeen, North Carolina Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org